

# UCHUNGUZI WA UTAMBUZI

Athari za Ufuatiliaji wa Mawasiliano kwa Watetezi wa Haki za Kibinadamu katika Kenya

NOVEMBA 2020

DEFENDERS COALITION

# SHUKRANI

Muungano wa Watetezi (Defenders Coalition) ungependa kuwashukuru watu wote waliochangia chapisho hili. Tunawashukuru kwa njia ya kipekee Patrick Mutahi na Brian Kimari, waliofanya utafiti na kuandika ripoti hii. Muungano wa watetezi pia unamshukuru na kumthamini Gloria Madegwa kwa kuongoza utafiti huu hadi mwisho wake.

Tunamshukuru kwa dhati Kamau Ngugi, mratibu mkuu kwa uongozi na mwongozo wake wa kimkakati kote katika kazi hii. Zaidi ya hayo tunatambua na kuthamini kwa dhati majukumu yaliyotekelezwa na Salome Nduta, Esban Muthoni, Francis Ndegwa na timu yote katika Muungano wa Watetezi kwa kutoa mchango wa kiteknolojia wa kubuni dhana ya mradi na maoni yao yenye thamani kubwa kwa utengenezaji wa mwisho wa chapisho hili.

Mwishowe, Muungano unatambua ujitoleaji thabiti wa bodi yetu ya wadhamini na washirika wa maendeleo. Mradi huu uliungwa mkono na Privacy International ambao tunawashukuru kwa kuwezesha uchapishaji wa ripoti hii.

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AU | Umoja wa Afrika |
| CDTD | Kituo cha Mafunzo ya Ndani na Maendeleo |
| CA | Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya |
| CCK | Tume ya Mawasiliano ya Kenya |
| CIGI | Kituo cha Uvumbuzi wa Utawala wa Kimataifa |
| CSO | Shirika la Jamii ya Kiraia |
| DPA | Sheria ya Ulinzi wa Data |
| HRC | Kamati ya Haki za Kibinadamu |
| HRD | Mtetezi wa Haki za Kibinadamu |
| ICCPR | Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa |
| ICRT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| ITU | Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano |
| KHRC | Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya |
| KNCHR | Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya |
| KICA | Sheria ya Habari na Mawasiliano ya Kenya |
| NGO | Shirika Lisilo la Kiserikali |
| NIIMS | Mfumo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Utambulisho Jumuishi |
| NIS | Huduma ya Ujasusi ya Kitaifa |
| UDHR | Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu |
| UN | Umoja wa Mataifa |

# YALIOMO


**Orodha ya Vifupisho** iv

**Muhtasari Mkuu** 7

**Utangulizi** 11

**Mbinu** 13

- Kuficha Majina, Usalama na Faragha 13
- Demografia ya Wahojiwa 14

**Matokeo na Uchanganuzi** 17

- Ulinzi wa kisheria wa faragha, habari na mawasiliano 17
- Mageuzi ya ufuatiliaji wa mawasiliano katika Kenya 20
- Ufahamu wa HRD wa faragha mtandaoni na ufuatiliaji wa mawasiliano 23
- Dhana muhimu zinazohusiana na ufuatiliaji wa mawasiliano 23
- Uzoefu wa usalama mtandaoni 24
- Dhana muhimu zinazohusiana na faragha ya mawasiliano 26
- Ufahamu wa taratibu na majukwaa ya ukusanyaji wa data 26
- Maarifa kuhusu ufuatiliaji wa mawasiliano 27
- Utambuzi wa HRD kuhusu matishio ya ufuatiliaji na faragha 28
- Vyanzo vya ufuatiliaji 28
- Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano 30
- Utambuzi wa ukusanyaji wa data za biometriki kwa huduma za serikali 31
- Utambuzi wa ukusanyaji wa data ili kushughulikia COVID-19 34
- Tabia na mazoea ya HRD mtandaoni 36
- Mitazamo ya habari za kibinafsi na za kikazi 36
- Nyayo za dijiti za HRD 37
- Mazoea na hatua za kiusalama mtandaoni 38

**Hitimisho** 40

Nyongeza ya 1: Orodha ya marejeo 42

Nyongeza ya 2: Dodoso la Uchunguzi 45

Nyongeza ya 3: Mwongozo wa Mahojiano ya kisifa 54

# ORODHA YA MICHORO NA MAJEDWALI


*Mchoro wa 1: Umri wa wahojiwa* 4

*Mchoro wa 2: Idadi ya miaka ya tajiriba katika kazi ya HRD* 5

*Mchoro wa 3: Kiwango cha juu zaidi cha elimu kilichofikiwa* 5

*Mchoro wa 4: Aina ya kazi ya HRD* 6

*Jedwali la 1: Maneno yanayohusiana na "ufuatiliaji wa mawasiliano"* 15

*Mchoro wa 5: Uzoefu wa HRD wa ufuatiliaji wa mawasiliano na mtandaoni* 17

*Mchoro wa 5B: Uzoefu wa usalama mtandaoni (2018)* 17

*Jedwali la 2: Maneno yanayohusiana na faragha ya mawasiliano* 18

*Mchoro wa 6: Ufahamu wa taratibu na majukwaa ya ukusanyaji wa data* 18

*Mchoro wa 7: Ufahamu wa ufuatiliaji wa mawasiliano* 20

*Mchoro wa 7B: Ufahamu wa ufuatiliaji wa mawasiliano (2018)* 21

*Mchoro wa 8: Vyanzo vya ufuatiliaji* 22

*Mchoro wa 9: Vyanzo amilifu vya ufuatiliaji* 23

*Mchoro wa 10: Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano* 24

*Mchoro wa 10B: Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano mnamo 2018* 25

*Jedwali la 3: Sababu za kutojisajili kwa Huduma Number* 26

*Mchoro wa 11: Utambuzi wa data inayokusanywa ili kushughulikia COVID-19* 30

*Mchoro wa 12: Mtazamo wa habari za kibinafsi na za kikazi* 31

*Mchoro wa 12B: Mitazamo ya habari za kibinafsi na za kikazi (2018)* 32

*Mchoro wa 13: Tabia za mtandaoni* 32

*Mchoro wa 14: Tabia za usalama mtandaoni* 33

*Mchoro wa 15: Uchunguzi wa tabia za kiusalama (2018)* 34

*Mchoro wa 16: Hatua za Ulinzi Mtandaoni* 35

# MUHTASARI MKUU

Uchunguzi huu ulianzishwa ili kutathmini kiwango cha ujuzi, uelewa na utambuzi wa Watetezi wa Haki za Kibinadamu (HRD) wa ufuatiliaji wa mawasiliano, vilevile kutambua mikakati yao ya kupunguza ufuatiliaji wa mawasiliano. Uliongozwa na maswali ya utafiti yenye upana kuhusu desturi na misingi ya kisheria inayotumika kuongoza haki ya faragha; mitindo inayojitokeza ya jinsi serikali inavyotumia sheria hizi na jinsi zinavyoathiri HRD na kazi yake; kiwango cha ujuzi wa HRD, uelewa na utambuzi wa ufuatiliaji wa mawasiliano; mikakati inayotumiwa na HRD ili kupunguza ufuatiliaji.

**Matokeo Muhimu:**

Matokeo kadhaa yamejumuishwa katika ripoti hii:

- HRD wana kiwango kikubwa cha ufahamu wa vipengele kadhaa vya ufuatiliaji wa mawasiliano, na matishio yake kwa kazi yao.
- Kuna vyanzo mbalimbali vya ufuatiliaji, huku waingiliji na walaghai wakidhaniwa kuwa chanzo kikubwa wakifuatiwa na huduma ya ujasusi, na watoa huduma za mawasiliano na Intaneti (ISP). Vyanzo vingine vilivyotambuliwa ni pamoja na wahalifu, waajiri, marafiki, kampuni za kibinafsi na familia.
- HRD hudhania mashirika na vikosi vya usalama kuwa wanaojaribu kufikia habari zao, pamoja na kuwatumia marafiki na jamaa kuwachunguza na kukusanya habari kuwahusu.
- Wengi wa HRD wanaamini kwamba tayari washakuwa chini ya ufuatiliaji wa mawasiliano kwa sababu ya kazi yao. Hii ni pamoja na kuunganishwa kwa mawasiliano ya simu kisiri na kuingia katika akaunti zao za mitandao ya kijamii na baruapepe kisiri.
- HRD wanafahamu tabia ambazo huenda zikawaweka katika hatari ya ufuatiliaji na wengi wao wamechukua hatua kuzipunguza. Mawasiliano ya ana kwa ana yanachukuliwa kuwa njia salama zaidi katika uchunguzi huu; kutuma baruapepe na arafa bila usimbaji kunadhaniwa kuwa kwa usalama wa chini kabisa.
- Njia za kawaida zaidi ambazo HRD hutumia kulinda vifaa vyao vya mawasiliano ni pamoja na utumiaji wa nywila ambazo wanabadilisha mara kwa mara, ugeuzaji wa mipangilio ya faragha ili kupunguza data ambazo zinaweza kufikiwa na vidakuzi; uangaliaji katika mitandao ya kijamii, ubadilishaji wa nywila wa mara kwa mara, ukaguzi wa mara kwa mara wa data ya kukusanywa, na utumiaji wa zana mbalimbali za mawasiliano.

- Kusita kupokea michango ya simu na kompyuta, kupata na kuficha nyayo pia zilikadiriwa juu. HRD pia wanatahadhari sana kile wanachoshirikisha mtandaoni.
- HRD wana wasiwasi kuhusu usalama na faragha ya habari zao za kibinafsi na zinazohusiana na kazi. Hata hivyo, kuna matokeo anuwai ya hofu mbalimbali na mapengo kati ya wasiwasi kuhusu ufuatiliaji mtandaoni na mazoea halisi ya ushirikishaji wa habari.
- Wengi wa HRD, ingawa wanafahamu Sheria ya Ulinzi wa Data, hawaelewi vizuri masharti na athari zake, likiwemo jukumu la Kamishna wa Data.
- Wengi wana wasiwasi kuwa data inayokusanywa kama sehemu ya hatua za kushughulikia janga la COVID-19 haiko katika mikono salama ya serikali au mashirika.

  HRD wanashuku data ya biometriki inayokusanywa na Mfumo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Utambulisho Jumuishi (NIIMS) au Huduma Number.

Mapendekezo

Kwa serikali:

- Harakisha marekebisho ya Sheria ya Utumiaji Mbaya wa Kompyuta na Jinai za Mtandaoni, 2018, ili kuhakikisha kufuatwa kwa Katiba na viwango vya kimataifa vya kulinda faragha.
- Tunga sera na sheria zinazotoa mazingira salama na ya kuwezesha kwa watetezi kuendesha kazi yao kwa uhuru na bila ufuatiliaji wa mawasiliano.
- Harakisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Data pamoja na kuhakikisha ofisi ya Kamishna wa Data inafanya kazi, ina rasilimali bora, na haiingiliwi.
- Chunguza matukio yanayoripotiwa ya ufuatiliaji haramu wa watetezi wa haki za kibinadamu na kuhakikisha kwamba watu wanaohusika wanachukuliwa hatua.
- Chukua hatua zinazohitajika ili kugeuza sera na mazoea ya ufuatiliaji kuhakikisha zinazingatia wajibu wa Kenya wa haki za kibinadamu wa kitaifa na kimataifa.
- Itisha uwajibikaji na uwazi wa mawakala wa utekelezaji wa sheria na usalama wanaofanya shughuli za ufuatiliaji
- Fichua uwezo wa ufuatiliaji wa serikali ya Kenya
- Anzisha hatua za kuhakikisha kwamba haki za wateja wa simu za mkononi kuhusiana na data yao ya kibinafsi zimehakikishwa;

Kwa sekta ya kibinafsi:

- Wawe na uwazi zaidi kuhusu mitindo yao ya biashara, vilevile jinsi data ya kibinafsi inavyochakatwa kama matokeo ya matumizi ya huduma zao;
- Waweke hadharani hatua wanazochukua kuitikia ombi la serikali la data ya kibinafsi ya watumiaji wao, kwa mfano, kupitia uchapishaji wa ripoti za uwazi.
- Wazingatie masharti ya Sheria ya Ulinzi wa Data kuhusu kuchakata, kuhifadhi na kushirikisha data inayohusu wateja wao.

Kwa Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya:

- Ombeni uteuzi wa mamlaka huru ya kuchunguza mipango ya ufuatiliaji wa mawasiliano inayoendeshwa na serikali ya Kenya na kuhakikisha kwamba mazoea hayo yanaheshimu wajibu wa kitaifa na kimataifa wa serikali wa kulinda faragha ya raia wake na data yao ya kibinafsi.
- Chunguzeni matukio yote yanayoripotiwa ya ufuatiliaji wa watetezi wa haki za kibinadamu na kuhakikisha taratibu za urekebishaji zinapatikana iwapo uchunguzi utapelekea utambuaji wa ukiukaji wa haki ya faragha.
- Teteeni upitishwaji wa hatua za kuhakikisha kwamba hali ya ufuatiliaji wa shughuli za mtandaoni na nje ya mtandao ni halali na hazikiuki haki ya watetezi wa haki za kibinadamu za uhuru wa kujieleza na uwezo wa kutetea haki za kibinadamu, pamoja na kupitia utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Kwa CSO na HRD wa kitaifa, eneo na kimataifa:

- Teteeni marekebisho ya Sheria ya Utumiaji Mbaya wa Kompyuta na Jinai za Mtandaoni, 2018 ili kuhakikisha kufuatwa kwa Katiba na viwango vya kimataifa vya kulinda faragha.
- Chunguzeni uanzishwaji na utekelezaji wa ofisi ya Kamishna wa Data na kuhakikisha uwezo wake, kulinda uhuru wake na kuhakikisha inazingatia sheria.
- Jihusisheni na utetezi unaolenga kuwajibisha ISP kwa sheria kwa kadiri ambavyo ufuatiliaji wa mawasiliano na faragha unahusika.
- Endeleeni kujenga uwezo wa kutambua matishio na hatari, na mkuze mikakati inayofaa ya kuzipunguza. Mashirika na mitandao inapaswa kufikiria upya mazoea ambayo huenda yakafunua HRD kwa ufuatiliaji na hatari za kiusalama.
- Hakikisheni ufuatiliaji wa mawasiliano na usalama wa habari ni mada za mazungumzo ya mara kwa mara katika majukwaa ya HRD kwani uko katika kiini cha kazi yao.

Kwa wafadhili:

- Ungeni mkono HRD na CSO ili kujenga mifumo, mipango na sera ambazo zinaweza kuboresha utekelezaji wa sera na mazoea salama ya mawasiliano.
- Toeni ufadhili kwa CSO walio mashambani ili kushughulikia masuala ya faragha na ufuatiliaji.
- Ungeni mkono juhudi za kulinda na kuhamisha kwa muda mfupi HRD walio katika mazingira ya mafadhaiko kwa sababu ya ufuatiliwaji wa mara kwa mara na kukumbana na matishio makali ya usalama kwa sababu ya kazi yao.
- Endeleeni kuunga HRD mkono ili kuwasiliana, pamoja na katika kiwango cha kimataifa. Hii ni pamoja na kuwasaidia baadhi ya HRD kushiriki katika majukwaa ya kieneo na kimataifa kama vile Tume ya Kiafrika ya Haki za Kibinadamu na taratibu za UN kama Wanahabari Maalum.

# UTANGULIZI

Haki ya faragha hufikiriwa kuwa haki ya kimsingi na imelindwa katika sheria kote ulimwenguni ikiwemo Kenya kama ilivyoelezewa katika Haki za Raia. Inaashiria "ile sehemu ya uhuru wa kibinafsi ambapo binadamu hujitahidi kupata kujitambua ... pweke au pamoja na wengine."[1] Mwanahabari Maalum wa UN wa Haki za Kibinadamu kuhusu Haki ya Kujieleza amewasilisha faragha kama uwezo wa watu binafsi kuamua ni nani anayemiliki habari kuwahusu na jinsi habari hiyo inavyotumiwa.[2] Kuhusu Kamati ya Haki za Kibinadamu ya UN, faragha, kama inavyofikiriwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, inarejelea "tufe la maisha ya mtu ambamo anaweza kuelezea utambulisho wake kwa uhuru, iwe ni kwa kuingia kwenye uhusiano na wengine au peke yake."[3] Haki ya faragha inajumuisha faragha ya habari, faragha ya kimwili, faragha ya mawasiliano, faragha ya kieneo, na ufuatiliaji.[4]

HRD wengi wa Kenya wamezusha wasiwasi kuhusu simu zao za mkononi kuunganishwa kisiri na mawasiliano yao kuingiliwa.[5] Kwa sababu ya maana hasi katika usalama wao na ule wa familia zao, matukio haya yamekuwa na athari ya kuogofya katika utekelezaji wa HRD wa haki za uhuru wa kujieleza, kujihusisha na kukusanyika. Ni muhimu kuhakikisha kwamba HRD wanaweza kufanya kazi yao bila hofu ya kusikilizwa, kuunganishwa kisiri, kuhifadhiwa au aina nyingine za uingiliaji au ufuatiliaji wa mawasiliano na data inayohusiana.

Ni lazima ufuatiliaji halali uazimie kufikia viwango vya chini vilivyotolewa katika Katiba, sheria za eneo na sheria na mikataba ya kimataifa ambayo Kenya inashiriki. Ni lazima watu binafsi walindwe dhidi ya uingiliaji wa kiholela wa haki yao ya kuwasiliana faraghani. Ni lazima hatua yoyote inayolenga kuingilia mawasiliano ichukuliwe tu kwa mujibu wa sheria, na iridhishe kwamba ni hatua nafuu na

1 Nowak, M. (1993) U.N. Agano Kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa: Ufafanuzi wa CCPR, (toleo la 2) Kehl am Rhein, Ujerumani; Arlington, VA: N.P. Engel Publishers.

2 Umoja wa Mataifa (2013) 'Ripoti ya Mwanahabari Maalum juu ya ukuzaji na ulinzi wa haki ya uhuru wa maoni na kujieleza, Frank La Rue' A/HRC/23/40, 17 Aprili 2013

3 http://www.humanrights.is/en/human-rights-education-project/comparative-analysis-of-selected-case-law-achpr-iachr-echr-hrc/the-right-to-respect-for-private-and-family-life/what-is-private-life

4 Tume ya Sheria ya Kivictoria katika Australia (2001) 'Sheria ya Faragha: Machaguo ya Mabadiliko', Gazeti la Habari, www.lawreform.vic.gov.au (Ilifikiwa mnamo 16 Januari 2018);
Privacy International, (2006) Faragha na Haki za Kibinadamu 2006: Uchunguzi wa Kimataifa wa Sheria na Maendeleo ya Faragha.

5 Shirika la Kutetea Haki za Kibinadamu (2017) "Haistahili Hatari" Matishio ya Uhuru wa Kujieleza Kabla ya Uchaguzi wa Kenya wa 2017," , https://www.hrw.org/sites/default/files/report_pdf/kenya0517_web.pdf

mwafaka kuhalalisha ukiukaji wa haki ya faragha.[6] Katika CORD dhidi ya Mkuu wa Sheria ilisemwa kwamba "...ufuatiliaji kwa namna ya kuingilia mawasiliano una athari katika faragha ya mtu kwa kumwacha mtu huyo wazi kwa tishio la kuwa wazi mara kwa mara. Hii hukiuka faragha ya mtu huyo kwa kuwawezesha wengine kuingilia nafasi yake ya kibinafsi na kufunua eneo lake la faragha."[7]

Ripoti hii inachanganua mahitaji, wasiwasi na mambo ya shauku kwa HRD kuhusiana na faragha, ulinzi wa data na ufuatiliaji wa mawasiliano. Pia inabaini jinsi ufuatiliaji unaathiri kazi ya HRD na jukumu lao kama watendaji wa mabadiliko katika jamii; na iwapo sheria, sera na hatua zinazopunguza haki ya HRD ya faragha zimefikia mahitaji ya kikatiba. Kazi ya haki za kibinadamu inahitaji utumiaji wa zana za mawasiliano kuanzia ana kwa ana, zana za kiasili za mawasiliano kama simu na sasa, zana za dijiti. Zote hizi hutoa viwango anuwai vya hatari, ambazo pia ni maalum kwa kazi ambayo HRD anahusika nayo, vilevile muktadha. Kuchunguza viwango vya hatari kulingana na mambo haya maalum vilevile kutafuta hatua zifaazo zaidi kutakuwa muhimu kwa ulinzi endelevu wa HRD. Mwishowe, ripoti hii inatoa mapendekezo kwa wahusika anuwai wakiwemo HRD ili kuwasaidia katika ukuzaji wa mikakati ya uingiliaji kati na utetezi.

---

6 Privacy International, 'Ufuatiliaji wa Mawasiliano. Video: Ufuatiliaji Wa Mawasiliano Ni Nini?' https://privacyinternational.org/explainer/1309/communications-surveillance

7 Muungano wa Mabadiliko na Demokrasia (CORD) na wengine 2 dhidi ya Jamhuri ya Kenya na wengine 10 [2015] eKLR, aya ya 290.

# MBINU

Uchunguzi huu ulitumia mbinu mseto, kuchanganya njia za kisifa na kikiasi. Jumla ya wahojiwa 56 wa HRD (wanawake 40; wanaume 16) kutoka kaunti 38 walifikiwa katika uchunguzi huu, huku HRD 10 wakihojiwa kama watoa-habari muhimu. Wahojiwa walichaguliwa kwa kufanya sampuli makusudi kutoka kwa hifadhidata ya Muungano wa Watetezi.

Data ya uchunguzi ilikusanywa kutumia njia ya Mahojiano kwa Simu Yanayotumia Kompyuta (CATI). Mbinu hii ya utafiti ni pale mhoji anapiga simu na kumsomea mhojiwa dodoso. Dodoso liliwekwa katika zana ya ukusanyaji data (Kobo Collect), ambayo ilikuwa na urukaji wa utaratibu kiotomatiki na mantiki nyingine yenye masharti, ambayo yalisaidia kulitekeleza kwa ufanisi. Baada ya kumtambua mhojiwa aliyeteuliwa kutoka kwa orodha iliyoteuliwa awali, mhoji alipiga simu iliyotolewa na mhojiwa bila mpangilio. Kwa kila nambari iliyotolewa, mhoji alijaribu kupiga simu mara tano, ambayo kama haikujibiwa ilimaanisha mtu huyo hakupatikana kwa mahojiano.

Watoa-habari muhimu walijibu maswali yaliyotayarishwa awali ya masuala ya faragha, uhuru wa kujieleza na habari. Mahojiano yaliwekwa kwenye maandishi na kutumiwa katika kuboresha uchanganuzi uliofanywa katika mapitio dawatini.

Mahojiano na uchunguzi wa watoa-habari muhimu yalitokana na upitiaji wa fasihi husika inayohusu ufuatiliaji wa mawasiliano. Utafiti katika eneokazi ulinasa machapisho husika kuhusiana na faragha, usalama na ulinzi wa HRD na wahusika wa kiserikali na wasio wa kiserikali katika Kenya. Ripoti iliongozwa na viwango vya haki za kibinadamu zilizowekwa na kuelezewa kwenye Katiba, maamuzi ya kortini, kanuni za kimataifa za mazoea ya HRD, kanuni na mkataba wa haki za kibinadamu, maazimio maalum ya UN, na ripoti za wataalamu akiwemo Mwanahabari Maalum kuhusu Hali ya Watetezi wa Haki za Kibinadamu.

### Kuficha Majina, Usalama na Faragha


Ikizingatiwa hali ya kazi hii, ufichaji wa majina ya wahojiwa ulikuwa muhimu na watafiti walitumia taratibu za kuondoa utambulisho ili kulinda data zao za kibinafsi. Katika ukusanyaji wa data, watafiti waliepuka ukusanyaji wa habari za kibinafsi zisizo muhimu na vitambulisho maalum ambavyo vingeonyesha wahojiwa. Data yao ilifichwa zaidi na kuhifadhiwa kwenye mafaili yaliyolindwa kwa nywila ambayo yangefikiwa na watafiti pekee.

Watafiti pia walipata idhini ya wahojiwa, na kujenga uaminifu na uelewano nao kabla ya kuendesha mahojiano ya kisifa. Pia walichukua hatua kuhakikisha usalama wa kimwili wa wahojiwa, na kufanya mahojiano katika sehemu zilizoidhinishwa kabla na Muungano wa Watetezi kuwa salama na za starehe kwa HRD.

### Demografia ya Wahojiwa

Wahojiwa walijitambulisha wenyewe kama HRD na wanafanya kazi kivyao au kupitia mitandao au mashirika kutetea na kukuza haki za kibinadamu. Kutokana na uchunguzi huu, asilimia 71 walijitambulisha kama wake na asilimia 29 kama waume. Wahojiwa walipatikana katika umri mbalimbali huku wengi wao (asilimia 45) wakiwa na umri wa kati ya miaka 18 na 30.

**UMRI**




*Mchoro wa 1: Umri wa wahojiwa*

Wengi wa HRD walihusishwa na au walifanya kazi na shirika wakati wa mahojiano na walikuwa na tajiriba ya kazi ya miaka 1-5.

MIAKA YA TAJIRIBA KATIKA KAZI YA HRD






*Figure 2: Years of experience in HRD work*

The survey respondents had attained different education qualifications with 80% having undertaken higher or post-secondary education in various disciplines.


KIWANGO CHA JUU CHA ELIMU




*Mchoro wa 3: Kiwango cha juu cha elimu kilichofikiwa*

Majibu ya uchunguzi yalijumuisha masuala ya ufuatiliaji na faragha yanayowaathiri HRD wanaoshughulikia masuala mbalimbali ya haki za kibinadamu.

Ni aina gani za masuala (yanayohusiana na haki za kibinadamu) umekuwa ukishughulikia?




*Mchoro wa 4: Aina ya kazi ya HRD*

# MATOKEO NA UCHANGANUZI

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya uchunguzi, kuonyesha utambuzi wa HRD wa ufuatiliaji wa mawasiliano.

**Ulinzi wa kisheria wa faragha, habari na mawasiliano**

Kifungu cha 31 cha Katiba ya Kenya ya 2010 kinahakikisha kwamba "Kila mtu ana haki ya faragha, ambayo ni pamoja na haki ya kutokuwapo kwa (a) upekuzi wake, nyumba au mali yake; (b) upokonyaji wa mali yake; (c) kutakikana pasipo haja au kufichuliwa kwa habari inayohusiana na shughuli za familia yake au za kibinafsi; au d) ukiukaji wa faragha ya mazungumzo yake." Walakini, haki ya faragha inapunguzwa kisheria lakini "kwa kadiri kwamba upunguzaji huo ni nafuu na wa haki katika jamii wazi na ya kidemokrasia yenye misingi ya hadhi ya kibinadamu, usawa na uhuru"[8] tu.

Sheria ya Habari na Mawasiliano ya Kenya (1998) inalinda haki za faragha ya mawasiliano na habari katika sehemu yake ya 31, ambayo inaifanya hatia kuingilia ujumbe uliotumwa kupitia huduma ya mawasiliano iliyo na leseni na kufichua maudhui yake, hatia hiyo ina adhabu ya kifungo cha miaka matatu gerezani au faini ya hadi shilingi elfu tatu za Kenya, au zote mbili. Sehemu ya 83W pia inaharamisha kitendo cha kupata makusudi ufikiaji usioidhinishwa wa mfumo wowote wa kompyuta kwa madhumuni ya kujipatia, moja kwa moja au vinginevyo, huduma yoyote ya kompyuta; na kitendo cha kuingilia, moja kwa moja au vinginevyo, kipengele chochote au data yoyote ndani ya mfumo wa kompyuta.

Waaidha, KICA ilirekebishwa na Kanuni za Habari na Mawasiliano za Kenya (Ulinzi wa Watumiaji) 2010, ambayo inazuia huduma za mawasiliano zenye leseni kuchunguza, kufichua au kukubalia mtu yeyote kuchunguza au kufichua, maudhui ya habari za mteja yeyote zinazosambazwa kupitia mifumo iliyo na leseni. Kanuni hizo zinapiga marufuku kihususa wenye leseni hao kusikiliza, kuunganisha kisiri, kuhifadhi au aina nyingine za uingiliaji au ufuatiliaji wa data za mawasiliano au zinazohusiana.[9] KICA pia inawezesha Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA) kushtaki hatia zote chini ya Sheria hiyo (sehemu ya 104).

Sheria ya Utumiaji Mbaya wa Kompyuta na Jinai za Mtandaoni, 2018 inashughulikia hatia zinazohusiana na mifumo ya kompyuta na uanzishwaji wa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Kompyuta na Jinai za Mtandaoni.[10] Zaidi, inataka (a) kulinda usiri, uadilifu na upatikanaji wa mifumo, programu na data ya kompyuta; (b) kuzuia utumiaji haramu wa mifumo ya kompyuta; (c) kuwezesha uzuiaji, ugunduzi, uchunguzi, mashtaka na adhabu ya jinai za mtandaoni; (d) kulinda haki za faragha,

8 Kifungu cha 24, Katiba ya Kenya 2010

9 Kifungu cha 15, Katiba ya 2010

10 Bado haijaanza kufanya kazi. Kamati inaanzishwa chini ya sehemu ya 27 ya Sheria, ambayo ilisimamishwa hadi 3 Februari 2020

uhuru wa kujieleza na ufikiaji wa habari kama ilivyohakikishwa chini ya Katiba; na (e) kuwezesha ushirikiano wa kimataifa kuhusu masuala yanayoshughulikiwa chini ya Sheria.

Kufuatia utekelezaji wake mnamo 16 Mei 2018, Ushirika wa Wanablogu wa Kenya (BAKE) uliwasilisha ombi la kikatiba mnamo Mei 29 2020 kuitaka Mahakama Kuu kutangaza kuwa sehemu 26 za Sheria hiyo zilikuwa kinyume cha katiba.[11] BAKE ilidai kwamba sehemu 5, 16, 17, 22, 23, 24, 27, 28, 29, 31, 32, 33, 34, 35, 36, 37, 38, 39, 40, 41, 48, 49, 50, 52, na 53 za Sheria hiyo zinakiuka uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari na haki ya faragha. Masharti haya yanashughulikia masuala mbalimbali ukiwamo uchapishaji wa habari za uongo, ponografia ya watoto, unyanyasaji mtandaoni, utapeli wa mtandaoni na usambasaji usiofaa wa picha chafu au za kisiri. Huku utekelezwaji wa masharti haya ukisimamishwa tangu 2018, korti ilitoa uamuzi mnamo 20 Februari 2020 na kutupilia mbali ombi hilo na kusema kwamba sehemu za Sheria hiyo zilizotiliwa shaka zilikuwa za haki chini ya Katiba na hazikukiuka haki na uhuru wa kimsingi. BAKE imewasilisha rufaa yake.[12]

Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2019 inaanzisha ofisi ya kamishna wa data ambaye amepewa mamlaka ya kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote yaliyo chini ya ulinzi wa data; na kukagua mashirika ya umma na ya kibinafsi ili kutathmini uchakataji wao wa habari na data ya kibinafsi. Inaweza kuanzisha tathmini hizi kivyake au kufuatia maombi ya shirika la kibinafsi au la umma.

Pamoja na ulinzi mwingine, Sheria ya Ulinzi wa Data Nambari 24 ya 2019 inashughulikia haki ya mtu — (a) kuarifiwa kuhusu jinsi data yake ya kibinafsi itakavyotumiwa; (b) kufikia data yake ya kibinafsi iliyo chini ya ulinzi wa mdhibiti wa data au mchakataji wa data; (c) kupinga uchakataji wa data yake ya kibinafsi, yote au sehemu yake; (d) kusahihisha data ya uongo au inayopotosha; na (e) kufuta data ya uongo au inayopotosha kuwahusu.

Wakati korti katika Jukwaa la Haki za Wanubi na wengine 2 dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 6 (2020)[13] ilipata kuwa Sheria ya Ulinzi wa Data Nambari 24 ya 2019 imejumuisha nyingi za kanuni mwafaka za ulinzi wa data, ilisema kwamba Sheria hiyo bado ilihitaji kutekelezwa kwa njia ya uteuzi wa Kamishna wa Data, na usajili wa wadhibiti na wachakataji data, vilevile uanzishwaji wa kanuni zinazofanya kazi. Tume ya Huduma za Umma (PSC) ilikuwa imeanza mahojiano mnamo 7 Julai 2020 na wagombea kumi walioteuliwa lakini mchakato huo ulilazimika kuanza upya baada ya kesi kuwasilishwa katika Korti ya Ajira na Uhusiano wa Leba ikilaumu PSC kwa kukosa kufuata utaratibu sahihi wa kuajiri kama ulivyoelezewa katika

11 Ushirika wa Wanablogu wa Kenya (BAKE) dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 3; Kifungu cha 19 Afrika Mashariki na mwingine (Watu wenye Shauku) [2020] eKLR, Ombi Nambari 206 la 2019

12 Ushirika wa Wanablogu wa Kenya (BAKE), Taarifa kwa vyombo vya habari 7 Mei 2020, https://www.blog.bake.co.ke/2020/05/07/we-have-appealed-the-high-court-decision-on-our-cybercrimes-case/ (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

13 Ukumbi wa Haki za Wanubi na wengine 2 dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 6; Jamii ya Masilahi ya Watoto na wengine 9 (Watu wenye Shauku) [2020] Ombi la 56, 58 na 59 la 2019 (Limejumuishwa) eKLR

Sheria ya Ulinzi wa data.[14] Mnamo 13 Oktoba 2018, rais Uhuru Kenyatta alimteua Immaculate Kassait kwenye wadhifa wa kamishna wa data. Yeye ni mkurugenzi wa awali wa elimu kwa wapiga kura katika Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Wakati asilimia 63 ya HRD waliohojiwa walijua kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Data, asilimia 80 hawakujua kuhusu ofisi ya Kamishna wa Data. Hii inaonyesha ukosefu wa ufahamu na uelewa wa maudhui ya DPA. Kuna haja basi ya kuifanya maarufu Sheria hii na masharti yake miongoni mwa HRD.

Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (MoICT) ilichapisha Sera ya Teknolojia ya Kitaifa ya Habari na Mawasiliano (ICT) ya 2019. Sera hiyo inaweka ICT katikati mwa ajenda ya kitaifa ya kiuchumi na inaupatia kipaumbele utumiaji wa ICT ili kufikia Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs) na Maono ya 2030,[15] sera ya muda mrefu ya maendeleo ya kitaifa ya Kenya, ambayo malengo yake ni pamoja na ufikiaji wa jamii ya habari na uchumi wenye maarifa. Sera hiyo inajitahidi kupata hili pamoja na kupitia kutoa mwongozo kuhusu ulinzi ulioboreshwa wa data, usalama mtandaoni, usalama wa mitandao na usalama wa habari.

Kenya pia inahusika na mikataba ya kieneo na kimataifa, na kanuni ambazo zina ulinzi wa haki ya faragha. Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu (UDHR) katika kifungu cha 12 inashughulikia ulinzi wa faragha, familia, nyumbani na mawasiliano ya watu binafsi dhidi ya uingiliaji haramu wa kiholela. Masharti ya UDHR pia yamo katika mikataba mingine ya kimataifa ambayo Kenya imeridhia. Hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), ambayo hulinda haki ya faragha katika Kifungu cha 17, na kuweka wajibu kwa Kenya kutumia sheria na hatua nyingine ili kuwezesha upigaji marufuku wa uingiliaji kama huo vilevile ulinzi wa haki ya faragha. Ufafanuzi wa jumla wa Kifungu cha 17 cha ICCPR unaeleza zaidi kwamba ufuatiliaji, uwe wa kielekroniki au vinginevyo, uingiliaji wa simu, telegrafu na njia nyingine za mawasiliano, uunganishaji wa nyaya na kurekodi mawasiliano kunafaa kupigwa marufuku.[16]

Kama ilivyowekwa katika Kifungu cha 2(5) cha Katiba, kanuni za jumla za sheria ya kimataifa na mkataba au kanuni yoyote iliyoridhiwa na Kenya itabuni sehemu ya sheria ya Kenya. Hii inamaanisha kwamba sheria na kanuni za kimataifa zinatumika Kenya moja kwa moja kiasi kwamba hazikiuki Katiba. Basi Katiba inalinda zaidi haki ya faragha kwa kuweka kinyumbani sheria na kanuni husika za kimataifa.

Katika kiwango cha Umoja wa Afrika (AU), Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu haushughulikii haki ya faragha. Mnamo 2019, Tume ya Afrika ilipitisha Tamko la Kanuni kuhusu Uhuru wa Kujieleza na Ufikiaji wa Habari katika Afrika, ambalo lina miongozo kuhusu haki ya faragha na ulinzi wa data katika Afrika. AU

14 Wakati wa kuandika ripoti hii, bado mchakato ulikuwa unaendelea

15 Hati ya Maono ya 2030 ya Kenya inaweza kupakuliwa katika http://www.vision2030.go.ke/about-vision-2030/

16 Kamati ya UN ya Haki za Kibinadamu (1998) Maoni ya Jumla ya CCPR Nambari 16: Kifungu cha 17 (Haki ya Faragha), Haki ya Kuheshimiwa kwa Haki ya Faragha, Familia, Nyumbani na Mawasiliano, na Ulinzi wa Heshima na Sifa, 8 Aprili 1988, https://www.refworld.org/docid/453883f922.html [ilifikiwa mnamo 19 Oktoba 2020]

ilianza kutumia Mkataba juu ya Usalama Mtandaoni na Ulinzi wa Data ya Kibinafsi mnamo 2014 lakini bado haijapokea maridhio 15 yanayohitajika ili uanze kutumika. Ni Morisi, Namibia, Gine, Senegali, Ghana, na hivi karibuni, Rwanda pekee ambao wameuridhia. Katika kiwango cha Jamii ya Afrika Mashariki, mataifa shiriki yalikubali Msingi wa Sheria za Mtandaoni mnamo 2008.

Nchi nyingi za Afrika ikiwamo Kenya zinakabiliana na utungaji wa sheria maalum na zifaazo juu ya udhibiti wa ukusanyaji, udhibiti na uchakataji wa data za kibinafsi. Pengo hili la kisheria ni hatari kwa muktadha wa ukuaji wa haraka wa teknolojia ambao wenyewe unaunda udhaifu mpya kwa faragha na ulinzi wa data.

**Mageuzi ya ufuatiliaji wa mawasiliano katika Kenya**

Licha ya ulinzi wa kisheria na kisera uliotajwa hapo juu, serikali ya Kenya imechukua hatua ambazo zinapanua uwezo na mazoea ya mawakala wa ujasusi na utekelezaji wa sheria, kwa njia ambazo zinaweza kupelekea uingiliaji haramu wa haki ya faragha. Wengi wa hawa walianzishwa kabla ya kuanza kutumika kwa DPA na hawakuwa chini ya mahitaji yake.

Mnamo 2012, Tume ya Mawasilano ya Kenya ilitangaza nia yake ya kushughulikia matishio ya usalama mtandaoni kwa kuanzisha NEWS, mpango wa Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU) ambao unawezesha mamlaka kufuatilia mawasilano ya kidijiti yanayoingia na yanayotoka.[17] Mnamo 2013, ilidaiwa kuwa kulikuwa na usakinishaji wa Blue Coat PacketShaper nchini. Blue Coat huwezesha ufuatiliaji wa maingiliano ya watumiaji katika programu kadhaa kama vile Facebook, Twitter, Google Mail na Skype.[18] Hatua hizi mbili zilizua kelele kutoka kwa vyombo vya habari, CSO na umma kwa jumla wakitaja uwezekano wa ukiukaji wa haki ya faragha.

Mnamo 2014, Kampuni kubwa ya mawasiliano Safaricom ilizawadiwa zabuni ya kukuza Mfumo Jumuishi wa Mawasiliano na Ufuatiliaji kwa Usalama wa Umma kwa polisi wa Kenya. Lengo la mradi huo, ambao ni kwa ushirikiano na Huawei Technologies, ni, pamoja na mambo mengine, kuwezesha mawakala wa usalama kuwasiliana vyema na kuimarisha uwezo wao wa kupigana na ughaidi.[19] Mradi huu wa mabilioni ya pesa ulipelekea kuangikwa kwa kamera 1,800 za CCTV zenye uwezo wa kutambua sura na mabamba ya magari katika sehemu muhimu za Nairobi na 300 Mombasa. Pia ilijenga kituo cha usimamizi na udhibiti ambapo maudhui kutoka kwa kamera za CCTV na vifaa vya mkononi yanawasilishwa kwa wakati halisi; mfumo wa mkutano wa video; unaounganisha vituo 195 vya polisi

17 Tume ya Mawasiliano ya Kenya (2012) 'Kenya na ITU zatia saini makubaliano ya kiutawala kwa ajili ya KE-CIRT/CC', 17 Februari, http://www.cck.go.ke/news/2012/KE- CIRT_signing.html (Ilifikiwa mnamo 17 Januari 2018)

18 Maabara ya Mwananchi (2013) 'Planet Blue Coat: Kuweka Ramani ya Udhibiti wa Kimataifa na zana za Ufuatiliaji, Muhtasari wa Uchunguzi, Nambari 13, Januari 2013, Chuo Kikuu cha Toronto, MUNK Shule ya Shughuli za Kimataifa, https://citizenlab.org/wp-content/uploads/2013/01/Planet-Blue-Coat.pdf (Ilifikiwa mnamo Accessed 17 Januari 2018)

19 Daily Nation. (2014, Mei 13). Kwa nini Ikulu ilimpigia simu mkuu wa Safaricom kuhusu ukosefu wa usalama. Daily Nation. www.nation.co.ke/news/Why-State-House-made-a-call-to-Safaricom-chief-over-insecurity/-/1056/2313756/-/ybd3dt/-/index.html

kwa intaneti ya kasi ya juu; ukuzaji wa mitandao wa 4G LTE18 kwa polisi na vituo 80 vya ardhini; na kuwatolea polisi vifaa 7,600 vya mawasiliano vyenye kadi za SIM na kipengele cha picha na video; na kuunganisha magari 600 ya polisi kwenye kituo cha usimamizi na udhibiti.[20]

Mradi huu wa ufuatiliaji ulisifiwa kwa kudaiwa kuongeza uwezo wa watekelezaji wa sheria kugundua na kuitikia uhalifu. Huawei pia ilisifiwa kwa kupunguza kiwango cha uhalifu kwa asilimia 46 Mombasa na Nairobi na kuongezeka kwa asilimia 13.5 kwa utalii wa kimataifa Kenya mnamo 2016.[21] Pia polisi wanadai kwamba mradi huo umesaidia katika kuwatambua wahalifu kwa kushtakiwa na kwamba baadhi ya magari yaliyoibwa yamerejeshwa kwa hisani ya kamera za ufuatiliaji zenye utambuzi wa mabamba ya magari katika miji hiyo miwili.[22]

Hata hivyo, wasiwasi ni kwamba mradi wa Mfumo Jumuishi wa Mawasiliano na Ufuatiliaji kwa Usalama wa Umma  unakiuka haki za faragha za umma. Watetezi wa haki za kibinadamu wanaonya kuhusu uwezekano wa kushirikishwa kwa data ya kibinafsi na wahusika wa tatu wakiwamo wahusika wa kigeni, uchakataji na ukusanyaji wa mawasiliano bila idhini ya watu binafsi, hatari za huduma za uhifadhi zisizo salama na ufikikaji kutoka nje usio na idhini, na uwezekano wa data kufutwa au kubadilishwa.[23] Uchunguzi wa 2019 na wanahabari wa Wall Street Journal ulipata kwamba mafundi wa Huawei katika Uganda na Zambia walikuwa wamesaidia serikali za Afrika kupeleleza wapinzani wao wa kisiasa katika matukio angalau mawili, ikiwa ni pamoja na kuingilia mawasiliano na midia zao za kijamii zilizosimbwa, na kutumia data ya simu zao kufuatilia shughuli zao.[24] Zaidi ya hayo mtandao wa kitaifa wa mawasiliano wa Ethiopia uliokuzwa na ZTE umeimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa serikali yao ambao umewafanya wananchi wateseke kwa mbinu kadhaa za unyanyasaji – uzimwaji wa intaneti wa mara kwa mara, ufuatiliaji unaolenga wanahabari na wanasiasa wa upinzani, uchujaji wa udhibiti uliokithiri na dhuluma za watu binafsi kwa kushirikisha maudhui ya mtandaoni. [25]

Ripoti nyingine pia zimerekodi utumiaji mbaya wa teknolojia na serikali ya Kenya

---

20 Kapiyo, V. na Githaiga, G. (2014) 'Je, ufuatiliaji ni suluhisho la matishio ya kiusalama Kenya?', https://giswatch.org/en/country-report/communications-surveillance/kenya

21 Huawei, "Ufuatiliaji wa Video kama Msingi wa "Mji Salama" katika," https://www.huawei.com/ke/industry-insights/technology/digital-transformation/video/video-surveillance-as-the-foundation-of-safe-city-in-kenya

22 Huduma ya Kitaifa ya Polisi (2019) usalama waimarishwa Mombasa, 5 Septemba. http://www.nationalpolice.go.ke/2015-09-08-17-56-33/news/297-surveillance-heightened-in-mombasa.html

23 Muungano wa Kitaifa wa Watetezi wa Haki za Kibinadamu-Kenya (NCHRD-K), Mtandao wa Masuala ya Kisheria na Kimaadili Kenya na Mtandao wa Masuala ya Kimaadili juu ya HIV na Ukimwi (KELIN), Mpango wa Paradigm, na Privacy International (2019) Haki ya Faragha katika, Upitiaji wa Kimataifa wa Ripoti ya Pamoja Kipindi cha 35 –Kenya, Juli 2019,  ukurasa wa 8

24 Parkinson, J., Bariyo, N. na Chin, J. (2019) "Mafundi wa Huawei Walisaidia Serikali za Kiafrika Kupeleleza Wapinzani wa Kisiasa," Wall Street Journal, 15 Agosti, https://www.wsj.com/articles/huawei-techncians-helped-african-governments-spy-on-political-opponents-11565793017

25 Ushuhuda wa Steve Feldstein (2020) mbele ya Usikilizwaji wa Tume ya Upitiaji wa Uchumi na Usalama  wa Marekani-China kuhusu  Malengo ya Kimkakati ya China katika Afrika  Mei 8, 2020, ukurasa wa 4.

katika kutazama na kufuatilia raia. Hii ni pamoja na kupitia: madai ya uwepo wa programu ya upelelezi ya NSO Group ya Kiisraeli katika ISP mbili za Kenya, Safaricom na SimbaNet;[26] madai ya uwepo wa "kisanduku cha kati" katika mtandao wa simu wa Safaricom, ambacho kinaweza kutumiwa kuathiri trafiki na kusaidia katika ufuatiliaji (majaribio baadaye yalitoa matokeo hasi ya kisanduku cha kati kuashiria kiliondolewa);[27] madai ya mifumo ya mawasilano ya moja kwa moja ya mawakala wa usalama wa kitaifa.[28]

Pia kumekuwa na wasiwasi kuhusu ufuatiliaji wa wanahabari na HRD usio na usawa na wa haramu na serikali ya Kenya,[29] hasa wale wanaoshughulikia masuala ya kutokujali kuhusu ghasia za baada ya uchaguzi na mauaji yasiyo ya kisheria; kukabiliana na ughaidi; uwajibikaji, kukabilana na ufisadi na ukaguzi wa kijamii, haki za kijinsia na uzazi; na haki za kumiliki ardhi.[30]

Katika ripoti yao ya 2017, Fuatilia, Kamata, Ua: Ndani ya Ufuatiliaji wa Mawasiliano na Kukabiliana na Ughaidi katika Kenya, Privacy International walielezea mbinu, zana na desturi za mazoea ya ufuatiliaji wa mawasiliano za polisi na mawakala wa mawasiliano wa Kenya. Inaangazia kimsingi utumiaji wa ufuatiliaji kwa shughuli dhidi ya ughaidi. Ripoti hiyo iliangazia jinsi maudhui na data ya mawasiliano inaingiliwa na jinsi data ya mawasiliano huingizwa kwenye mizunguko ya ukamataji, mateso na utowekaji wa lazima. Hii ni pamoja na kupitia ushirikiano na kampuni za mawasiliano ambazo hutoa data maalum ya mteja makusudi kwa mawakala wa ujasusi na utekelezaji wa sheria bila kufuata njia sahihi. Pia inadai kwamba NIS ina ufikiaji wa moja kwa moja wa mitandao, hivyo kuwawezesha kuingilia mawasilano bila kampuni za mawasilano kujua.[31] Pia ilidai kuwa huenda NIS ikawa na kifaa ambacho kinaonekana kufanya kazi kama kinasa IMSI, ambacho ni kifaa cha ufuatiliaji wa simu kinachoweza kuingilia mawasiliano kiamilifu 'toka hewani' ya vifaa vilivyo karibu na kufuatilia mawasiliano ya sauti yanayoendelea, arafa zinazotumwa, na eneo la simu.[32]

Sehemu ya 69 ya sheria za Usalama (marekebisho) inarekebisha Sheria ya Uzuiaji wa Ughaidi ili kuruhusu uingiliaji wa mawasiliano na asasi za usalama wa nchi kwa madhumuni ya kugundua, kuzuia na kuvuruga ughaidi. Kwa mujibu wa Sehemu ya

26 Marczak, B., Scott-Railton, J., McKune, S., Abdul Razzak, B. na Deibert, R. (2018) Kibemasa: Ufuatiliaji wa Shughuli za Programu ya Kiujasusi ya NSO Group ya Pegasus katika nchi 45, Ripoti nambari 113 ya Utafiti wa Maabara ya Mwananchi, Chuo Kikuu cha Toronto, Septemba 2018.

27 Kituo cha Mali za Kitaaluma na Teknolojia ya Habari (2017) "Safaricom na ugeuzaji wa Trafiki ya Intaneti," Machi 2017, https://blog.cipit.org/wp-content/uploads/2017/03/Final-March-Brief-pages.pdf

28 Privacy International (2017) 'Fuatilia, Kamata, Ua: Ndani ya Ufuatiliaji wa Mawasiliano na Kukabiliana na Ughaidi katika Kenya', Privacy International.

29 https://privacyinternational.org/state-privacy/1005/state-privacy-kenya#commssurveillance

30 Brigedi za Amani za Kimataifa (2012) Tathmini ya uwezekano na ufanisi wa msindikizo wa kiulinzi katika Kenya https://peacebrigades.org.uk/fileadmin/user_files/international/files/special_report/PBI_Kenya_report.pdf

31 Privacy International (2017) Fuatilia, Kamata, Ua: Ndani ya Ufuatiliaji wa Mawasiliano na Kukabiliana na Ughaidi katika Kenya,

32 Privacy International (2017) Fuatilia, Kamata, Ua: Ndani ya Ufuatiliaji wa Mawasiliano na Kukabiliana na Ughaidi katika Kenya, ukurasa wa 27

36 ya Sheria ya Uzuiaji wa Ughaidi, uingiliaji huo unahitaji idhini kutoka Mahakama Kuu. Sheria ya Huduma ya Ujasusi ya Kitaifa (NIS) inaruhusu uingiliaji pakiwa na haki ya faragha kadiri kwamba NIS inaruhusiwa kuchunguza, kufuatilia au kuingilia vinginevyo watu walio chini ya uchunguzi wa huduma hiyo au wanaoshukiwa kufanya uhalifu, chini ya mamlaka yanayotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NIS.[33] Hii ina uwezekano wa kuwezesha ukiukaji wa faragha bila ukaguzi, katika kuhudumia maslahi ya serikali ambapo watu hao huenda wakashtakiwa kwa kufanya makosa hayo kama inavyoshughulikiwa katika Sheria ya NIS. Uwezekano wa upangaji wa habari kuhusu NIS kwa madhumuni ya usalama pia unaleta matishio ya ufuatiliaji na usalama kwa HRD.

Hata hivyo, katika Muungano wa Mabadiliko na Demokrasia (CORD) na wengine 2 dhidi ya Jamhuri ya Kenya, Mahakama Kuu iliamua kwamba ikizingatiwa hali ya ughaidi na hali na ustadi wa mawasiliano ya kisasa, uingiliaji wa mawasiliano na utafutaji ulikuwa wa haki na ilionekana hakukuwa na mbinu mbadala zisizo na vizuizi, za kufikia lengo la kiusalama lililokusudiwa.[34] Pamoja na hayo, mahakama ilielezea imani yake katika ulinzi uliotungwa ili kuzuia ukiukaji wa haki ya faragha wa kiholela.[35] Hii inaweka kitangulizi hatari ambacho huenda kikawezesha mawakala wa usalama kuepuka hitaji la kikatiba la kudhihirisha kwamba uzuiaji ulikuwa wa haki, wa lazima na wenye usawa.

### Ufahamu wa HRD wa faragha mtandaoni na ufuatiliaji wa mawasiliano

Dhana muhimu zinazohusiana na ufuatiliaji wa mawasiliano

Walipoulizwa ni nini huja akilini wasikiapo ufuatiliaji wa mawasiliano, wengi wa HRD walisema unaashiria uunganishaji kisiri au ufuatiliaji wa mawasiliano.


Kwa ujumla, kuna ufahamu miongoni mwa HRD kwamba ufuatiliaji unahusiana na ufikiaji wa mawasiliano, habari na data. Matokeo sawa yalirekodiwa katika ripoti ya utambuzi ya 2018, ambayo pia iliashiria kwamba HRD hasa walitambua utazamaji, ujasusi, ufuatiliaji, uunganishaji kisiri, upelelezi, polisi, uingiliaji na faragha kama maneno yanayohusiana na ufuatiliaji.

33 Sheria ya Huduma ya Ujasusi ya Kitaifa, sehemu ya 36 and42,

34 Coalition for Reform and Democracy (CORD) & 2 others v Republic of Kenya &10 others [2015] eKLR. See para 52

35 Coalition for Reform and Democracy (CORD) & 2 others v Republic of Kenya &10 others [2015] eKLR, para 303

Unaposikia maneno UFUATILIAJI WA MAWASILIANO, ni MANENO gani huja akilini mwako (Kwanza)





*Jedwali la 1: Maneno yanayohusiana na "ufuatiliaji wa mawasiliano"*

## Uzoefu wa usalama mtandaoni

Nusu ya wahojiwa wanaamini kuwa washafanyiwa uingiliaji haramu wa baruapepe na/au uunganishaji kisiri wa simu. Wakati baadhi ya HRD walielezea, katika mahojiano ya kisifa, kwamba walikuwa wamepokea mafunzo kiasi au walikuwa na maarifa kuhusu jinsi ya kuthibitisha kwamba wako chini ya ufuatiliaji, wengi hawakuwa wamepokea mafunzo kama hayo na walielezea kwamba waligundua walikuwa chini ya ufuatiliaji kwa kukagua mienendo na majibu ya mawakala wa usalama na wahusika wengine. Katika matukio mengi, hii ilikuwa kufuatia uvurugaji wa kazi yao ya HRD hata baada ya kuchukua hatua za kulinda habari hiyo na kuwasiliana tu na watu wanaoaminika.[36]


36 Mahojiano na SL, HRD, Oktoba 2020; Mahojiano na GA, HRD, Oktoba 2020

Je una sababu yoyote ya kuamini kwamba huenda lolote kati ya yafuatayo lilikufanyikia?




*Mchoro wa 5: Uzoefu wa HRD wa ufuatiliaji wa mawasiliano na mtandaoni*

Mnamo 2018, wengi wa HRD pia waliamini kwamba baruapepe, mitandao ya kijamii na simu zao zilikuwa zimeingiliwa pia.




*Mchoro wa 5B: Uzoefu wa usalama mtandaoni (2018)*

Baadhi ya HRD wakiwamo wanahabari pia walielezea kwamba wanaamini watawekwa chini ya ufuatiliaji kulingana na umuhimu wa kazi wanayofanya. HRD mmoja alielezea hivi: "Hasa kama unajulikana kwa kufanya kazi au makala yanayohusiana na ufisadi au uchaguzi, tunatarajia kwamba tayari simu zetu zimeunganishwa kisiri na mara nyingi tuko sahihi kuhusu hilo, hata maafisa wa polisi wakati mwingine wanakiri hilo kwetu au kutuonya."[37]

37 Mahojiano na JM, HRD, Oktoba 2020

## Dhana muhimu zinazohusiana na faragha ya mawasiliano


Wahojiwa waliombwa kutambua dhana moja inayokuja akilini wanaposikia kuhusu maneno 'faragha ya mawasiliano'. Wengi waliashiria maneno yanayohusiana na usiri wa mawasiliano yao.




*Jedwali la 2: Maneno yanayohusiana na faragha ya mawasiliano*

## Ufahamu wa taratibu na majukwaa ya ukusanyaji wa data


Kwa ujumla, unaweza kukadiriaje kiwango cha ufahamu/ maarifa yako juu ya matishio na hatari zinazoletwa na yafuatayo katika ufuatiliaji?




*Mchoro wa 6: Ufahamu wa taratibu na majukwaa ya ukusanyaji wa data*


Kama data inavyoonyesha, wengi wa wahojiwa wana maarifa ya juu kuhusu njia mbalimbali za ufuatiliaji kama inavyoonekana katika asilimia zilizojumuishwa zilizowekwa alama ya "juu" na "juu sana". Tofauti tu ni Mfumo wa nafasi wa Kimataifa (GPS), ambao asilimia 50 walisema walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu jinsi unavyotumiwa kwa ufuatiliaji. Hii ni sehemu iliyo na uwezekano kwa Muungano wa Watetezi kuangazia ujengaji wao wa uwezo.

**Maarifa kuhusu ufuatiliaji wa mawasiliano**




*Mchoro wa 7: Ufahamu wa ufuatiliaji wa mawasiliano*

Wengi wa wahojiwa wana maarifa wastani kuhusu vipengele mbalimbali vilivyojaribiwa. Wakati wengi wanajua jinsi ya kuhifadhi habari za kibinafsi kwa usalama, asilimia ya juu wana ufahamu wastani wa jinsi serikali inavyokusanya habari za kibinafsi, ufuatiliaji wa intaneti na ufuatiliaji wa mawasiliano.





*Mchoro wa 7B: Ufahamu wa ufuatiliaji wa mawasiliano (2018)*

Majibu kutoka kwa uchunguzi wa 2018 yanaashiria kwamba asilimia 57 ya HRD walijitambua kuwa na maarifa mengi kuhusu jinsi ya kuhifadhi habari kwa usalama na njia ambazo kwazo intaneti inaweza kufuatiliwa, na asilimia 50 walikadiria maarifa yao wenyewe ya ufuatiliaji wa mawasiliano kama juu ya wastani. Kama mnamo 2018, wahojiwa katika mahojiano ya kisifa walitaja ushiriki endelevu katika mafunzo mbalimbali juu ya usalama wa dijiti yanayoendeshwa na asasi anuwai za kiraia ikiwamo Muungano wa Watetezi na Privacy International. Hizi ni hatua chanya za Kuongeza ujuzi na maarifa ya HRD juu ya ufuatiliaji wa mawasiliano na kupunguza matishio wanayokabiliana nayo.

## Utambuzi wa HRD kuhusu matishio ya ufuatiliaji na faragha


Vyanzo vya ufuatiliaji




*Mchoro wa 8: Vyanzo vya ufuatiliaji*

HRD walitambua matishio ya ufuatiliaji wao yanaibuka kwa njia kubwa kutokana na matapeli na waingiliaji (asilimia 55), watoa huduma za intaneti/mawasiliano (asilimia 52), huduma za ujasusi (asilimis 50) na polisi (asilimia 47). Marafiki (asilimia 48) na jamaa (asilimia 46) pia waliashiriwa kuwa na uwezekano wa chanzo cha ufuatiliaji na HRD mmoja alielezea kwamba mara nyingi huwa wanapewa hongo na/au kutishwa na wahusika wengine ili kufuatilia habari zao za kibinafsi.[38]

Mnamo 2018, HRD walifahamu huduma za ujasusi kama uwezekano mkubwa wa chanzo cha ufuatiliaji (asilimia 53) ikifuatiwa na polisi (asilimia 37), na watoa huduma za mawasiliano au intaneti (asilimia 37).





*Mchoro wa 9: Vyanzo amilifu vya ufuatiliaji*

38 Mahojiano na GA, Oktoba 2020.

Ni jambo la kuvutia kwamba huku HRD wakihisi kwamba mashirika na vikosi vya usalama vinajaribu kufikia habari zao, wanaamini ni jamaa zao ambao wanawafuatilia. Hii inapendekeza uelewa kwamba marafiki na jamaa wana ufikiaji rahisi wao na vifaa vyao.


## Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano

Kwa maoni yako, njia zifuatazo za mawasiliano ziko salama kwa kiasi gani?




*Mchoro wa 10: Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano*

Kama tu uchunguzi wa 2018, wahojiwa walihisi kwamba mazungumzo ya ana kwa ana ndiyo njia salama zaidi ya mawasiliano ikifuatiwa na utumiaji wa rununu zilizosimbwa. Hata hivyo, walihisi hawako salama kwa kutuma arafa, kutuma baruapepe zilizosimbwa kuchapisha kwenye mitandao ya kijamii na kupiga simu. Huu ni mtazamo tofauti na wa 2018 ambapo HRD waliohojiwa walihisi kwamba kutuma arafa na kuchapisha kwenye mitandao ya kijamii kulikuwa njia za mawasiliano zenye hatari kidogo.




*Mchoro wa 10B: Utambuzi wa usalama wa zana na majukwaa ya mawasiliano mnamo 2018*


Majibu haya yanaashiria kwamba wahojiwa wanaelewa bayana maana ya ulinzi wa zana za mawasiliano na wanahusisha kwa usahihi baadhi ya maneno muhimu na usalama na ufuatiliaji wa mawasiliano. Katika ripoti hii, usimbaji inamaanisha mchakato wa kugeuza habari au data kuwa msimbo, hasa kwa kuzuia ufikiaji usioidhinishwa,[39] na usalama au ulinzi wa habari inamaanisha hatua zinazotumiwa na watu binafsi na/au mashirika kuhakikisha kwamba habari zao haziwezi kuingiliwa na watu wowote wasio na idhini. Unahusisha uhusiano kati ya ukusanyaji na usambazaji wa data na teknolojia, utambuzi na matarajio ya umma ya faragha na misingi ya kisiasa na kisheria inayozunguka data hiyo.[40] Pia unalenga kupata usawa kati ya haki za usalama za kibinafsi huku ukiruhusu data kutumiwa kwa madhumuni ya kibiashara.

### Utambuzi wa ukusanyaji wa data za biometriki kwa huduma za serikali

Sheria ya Sheria ya Bunge (Marekebisho Anuwai), 2018 (SLMAA) ilirekebisha Sheria ya Usajili wa Watu ili kuunda Mfumo wa Kitaifa wa Udhibiti wa Utambulisho Jumuishi (NIIMS), maarufu kama huduma number. Mfumo huu unaruhusu serikali kukusanya data nyingi kuhusu Wakenya na wageni waliosajiliwa kwenye hifadhidata ya kitaifa ikiwamo: nambari ya marejeleo ya ardhi na nyumba, data ya biometriki kama vile alama za vidole, jiometria ya mkono, jiometria ya ndewe, miundo ya retina na airisi, mawimbi ya sauti na DNA katika hali ya dijiti.

39 Needham, Roger M., na Michael D. Schroeder. "Kutumia usimbaji kwa uthibitishaji katika mitandao mikubwa ya kompyuta." Mawasiliano ya ACM 21.12 (1978): 993-999.
40 Bygrave, L. A. (2000) Sheria ya ulinzi wa data. Wolters Kluwer Sheria na Biashara, 2002.

Wakati NIIMS huenda ilikusudiwa kuimarisha utoaji huduma, inatoa matishio kadhaa kwa haki ya faragha. Kwa kweli, walipoulizwa ni kwa nini hawakujisajili kwa Huduma number, masuala ya faragha yalikuwa ya wasiwasi mkubwa kwa HRD.




Teknolojia za biometriki hutumia tabia au sifa za kipekee na za kudumu za kimwili kumtambua mtu binafsi. Mtu huyo anaposajiliwa katika mfumo huo – kwa mfano, mfumo wa kitaifa wa utambulisho – tabia ya biometriki inanaswa na kugeuzwa kuwa kigezo cha dijiti cha kuhifadhiwa kwenye mfumo kwa marejeleo ya baadaye na kulinganishwa ili kumtambua mtu huyo au mtu anayetakikana.[41] Kama ilivyoamuliwa katika Mtandao wa Kisheria na Kimaadili juu ya HIV na UKIMWI (KELIN) na wengine 3 dhidi ya Katibu wa Baraza Wizara ya Afya na wengine 4 [2016] eKLR kuhusu vipengele vyenye shida vya hifadhidata za serikali, "hata wakati ambao lengo linalofuatiliwa na Serikali ni halali, njia ambayo kwayo data inakusanywa inaweza kuwa na ukiukaji wa faragha." [42]

Hivyo basi, ukusanyaji wa data hiyo unahitaji kufanywa kwa mujibu wa sheria, kwa uangalifu mkubwa, na kwa idhini ya wahusika wa data hiyo kama ilivyoshughulikiwa sasa chini ya sehemu 30(1) ya Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2019. Mambo hayakuwa hivyo kwa NIIMS kwani hitaji la kujisajili kwa NIIMS lilifanywa bila kushauriana na umma na likafanywa la lazima. Umma, ambao ndio wahusika wa data kwa suala hili, basi hawakuidhinisha uchakataji wa data yao ya kibinafsi na muhimu. Hitaji la kutoa ramani za Mfumo wa Nafasi wa Kimataifa (GPS) pia lilikuwa la kiholela. Kuna uwezekano wa hii kutumika kufuatilia na kufanya ufuatiliaji mkubwa wa watu katika Kenya. Wakati baadhi ya HRD walijisajili kwa Huduma Number, wengi walisema kwamba hii kwa kiwango kikubwa ilikuwa ni kwa sababu ya hofu kwamba huenda wangenyimwa huduma za umma kama ilivyokuwa imetishiwa na Wizara ya Ndani na Uratibu wa Serikali.[43] Kama sehemu ya mikakati yao ya ulinzi, baadhi ya HRD walijisajili kwa Huduma Number lakini wakaacha baadhi ya habari muhimu au wakaweka habari za uongo makusudi.[44]

41 Bygrave, L. A. (2000) Sheria ya ulinzi wa data. Wolters Kluwer Sheria na Biashara, 2002.

42 Mtandao wa Kisheria na Kimaadili juu ya HIV na UKIMWI (KELIN) na wengine 3 dhidi ya Katibu wa Baraza Wizara ya Afya na wengine 4 [2016] eKLR

43Mahojiano na NC, Oktoba 2020

44 Mahojiano na SL, Oktoba 2020

Hifadhidata za data ya biometriki kama NIIMS pia inatoa matishio makali ya faragha. Kwanza, ufikiaji haramu wa hifadhidata kuu unaweza kutoa matishio makali ya usalama kwa nchi na raia wake na kukiuka haki za kikatiba. Hifadhidata hizo husimamiwa na watu na basi kushiriki katika kasoro za watu binafsi, huenda zikaingiliwa au kupatwa na uvujaji wa data. Mashahidi wataalamu katika Jukwaa la Haki za Kinubi na wengine 2 dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 6; Jamii ya Masilahi ya Watoto na wengine 9 (watu wenye shauku) [2020] eKLR kwa mfano walitoa ushahidi wa kasoro za ubunifu na majenzi za NIIMS wakidai kwamba kama mifumo mingine sawa kama vile Aandhar katika India, ingewafunua Wakenya kwa maovu kadhaa ukiwamo ufikiaji haramu. Ukusanyaji wa data za biometriki pia ulichukuliwa kuwa na uwezekano wa kutoa tishio kwa HRD, kazi yao na jamii ambako wanafanyia kazi/ambayo wanafanya kazi nayo, hili hasa kwa wale wanaofanya kazi na wachache wa kingono na kijinsia.[45]

Pili, uwezekano wa kuunganisha data ya kipekee ya mtu binafsi katika hifadhidata tofauti za kiserikali au kibinafsi kwa nambari moj unawezesha habari zote kuhusu mtu binafsi kufikiwa katika hifadhidata nyingi. Wizara ya ndani ilisifu NIIMS kama "chanzo kimoja cha ukweli (duka moja la kila kitu) cha data ya utambulisho wa mtu kwa raia na raia wa kigeni wanaoishi Kenya."[46] Wakati ni kawaida na hata kunahimizwa kwamba asasi za umma zishirikishe data ili kupunguza gharama na kuimarisha ufanisi, ni lazima haki za kibinafsi zizingatiwe. Ufikiaji wa data ya kibinafsi na maafisa wasioidhinishwa huenda ukamdhuru mtu binafsi. Kwa mfano, programu na programu-tumizi nyingi zinazofikiwa wazi zinatumika kunakili data ya alama ya vidole na sauti kwa wizi wa utambulisho. Basi mifumo ya data nyingi inafaa kutumika wakati tu, kwa njia dhahiri, ni lazima na yenye usawa ili kufikia lengo halali.[47]

Ikizingatia iwapo NIIMS ilikiuka haki ya faragha, Mahakama Kuu katika kesi ya Jukwaa la Haki za Wanubi iliamua kwamba "ukusanyaji wa DNA na ramani za GPS, kwa kufuata marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Watu yaliyotiliwa shaka, una uingiliaji na si wa lazima, na una ukiukaji wa Kifungu cha 31 cha Katiba". Mnamo Septemba 2020, Karanja Kibicho, katibu wa kudumu katika Wizara ya Ndani alifichua katika mkutanao mbele ya kamati ya bunge juu ya Sheria Iliyokabidhiwa kwamba serikali iko tayari kuanza awamu ya pili ya usajili kwa Huduma Number unaolenga makundi ambayo hayakusajili wakati wa zoezi la 2019.

45 Kwa ujumla biometriki hutoa matishio mengi hasa kwa sababu sisi hufanya kazi na wachache wa kingono na kijinsia.

46 Jukwaa la Haki za Wanubi na wengine 2 dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 6; Jamii ya Masilahi ya Watoto na wengine 9 (Watu walio na Shauku) [2020] eKLR, aya ya 329)

47 Kamati Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa (2004) Maoni ya Jumla Nambari 31 [80] Hali ya Wajibu wa Kijumla wa Kisheria Uliowekwa kwa Nchi Zilizo Washiriki wa Aganot, 29 Machi 2004 (mkutano wa 2187), CCPR/C/21/Rev.1/Add. 13, aya ya 6

**Utambuzi wa ukusanyaji wa data ili kushughulikia COVID-19**

Ili kusaidia katika ufuatiliaji wa waasiliani wakati wa janga la COVID-19, serikali ya Kenya kama mataifa mengine inatumia teknolojia. 'Kenya COVID-19 tracker', programu ya serikali ya kufuatilia COVID-19,[48] inawezesha timu za ufuatiliaji wa ugonjwa huo kusajili waasiliani, kuripoti matukio yanayoshukiwa ya COVID-19 kwa timu ya kitaifa ya ufuatiliaji, na kufanya uchunguzi wa matukio yanayoshukiwa. Programu hiyo hufanya kazi nje ya mitandao na inaingiliana na KenyaEMR. Mifumo hiyo miwili kwa pamoja inasaidia mtiririko wa kazi kwa usajili wa matukio, orodha ya waasiliani, ufuatiliaji, uchunguzi, oda za maabara ya COVID-19 na ushirikishaji wa data na maabara.[49]

Serikali pia ilizindua Jitenge, programu ya rununu kama moduli ya Mfumo wa Arifa na Ripoti za Dharura (EARS) unaotumika na Kituo cha Shughuli za Dharura cha Wizara ya Afya kuitikia zaidi ya magonjwa 40 yenye maambukizi. Jitenge inawawezesha watu kujisajili au kusajiliwa na maafisa anuwai wa Wizara ya Afya katika kituo cha uanzishwaji wa karantini kwa karantini ya nyumbani, katika majengo ya karantini na sehemu za kuingilia na maafisa wa kiafya wa bandari. Basi watumiaji waliosajiliwa wanapokea vikumbusho na vichocheo vya kila siku kuripoti juu ya hali yao ya afya zikiwamo dalili au taarifa nyingine yoyote. Mfumo huo unatumiwa kudhibiti na kufuatilia – utunzaji na udhibiti wa kinyumbani; karantini ya kibinafsi kwa waasiliani; ufuatiliaji baada ya kujitenga na ufuatiliaji wa madereva wa malori ya masafa marefu.[50]

Basi serikali ya Kenya imekuwa ikitumia zana za rununu na vyanzo vya data kwa shughuli za ufuatiliaji wa COVID-19, kama vile kufuatilia maambukizi na uenezaji katika jamii, kutambua maeneo yenye watu wengi yaliyo katika hatari na kutekeleza amri za karantini. Wizara ya Afya pia imekuwa ikisambaza arafa kuhusu COVID-19 na asilimia 79 ya wahojiwa wa uchunguzi huu wamepokea arafa kama hizo.

Utumiaji wa programu za rununu za ufuatiliaji wa waasiliani kwa ufuatiliaji wa waasiliani unatoa manufaa kadhaa; hazitegemei kumbukumbu za mgonjwa (ambaye huenda akawa mahututi wakati wa mahojiano); huwezesha waasiliani wasiojulikana na mgonjwa kufuatiliwa (k.m. abiria wenzake ambao waliketi karibu naye kwenye treni); zina uwezo wa kuharakisha mchakato; huenda zikasaidia ufuatiliaji zaidi wa waasiliani na mamlaka ya afya kupitia mfumo wa ujumbe. Kipengele cha ukaguzi wa dalili kinaweza kusaidia hii, lakini si muhimu.[51]


Hata hivyo, uwezekano wa manufaa ambayo zana za ufuatiliaji wa afya ya umma

48 Kenya COVID-19 Tracker, https://play.google.com/store/apps/details?id=org.medicmobile.webapp.mobile.surveillance_covid19_kenya&hl=en&gl=US

49 Medic Mobile (2020). "Habari Mpya Kuhusu COVID-19: programu inayoendeshwa na CHT inasaidia ufuatiliaji wa COVID-19 katika Kenya," 30 Aprili,

50 mHealth Kenya (2020) "Ufuatiliaji wa Afya ya Umma na Mifumo ya Uitikiaji," https://www.mhealthkenya.org/covid-19

51 Kituo cha Ulaya cha Uzuiaji na Udhibiti wa Magonjwa (2020) Ufuatiliaji wa waasiliani kwa ajili ya COVID-19: ushahidi wa sasa, machaguo ya kuimarisha na kutathmini rasilimali zinazohitajika, Ripoti ya Kiufundi, Aprili 2020, ukurasa wa 5





*Mchoro wa 11: Utambuzi wa data inayokusanywa ili kushughulikia COVID-19*

wa COVID-19 zilizoimarishwa kwa rununu zinatoa pia unaandamana na uwezekano wa madhara. Kuna hatari kuu kwa raia kutokana na ukusanyaji wa data muhimu, zikiwamo afya ya kibinafsi, mahali na data ya mawasiliano. Serikali ya Kenya haijafichua ni nani atakayepokea data ya COVID-19, jinsi wapokeaji hao wanaweza kuitumia na/au kuishirikisha na wengine. Pia si dhahiri ni hatua gani zitachukuliwa kulinda data hiyo dhidi ya wizi au matumizi mabaya kwani Sheria ya Ulinzi wa Data haijaanza kutekelezwa. Wengi wa HRD hawaamini kwamba serikali au mashirika yatahifadhi data yao salama.

Usipodhibitiwa, ukusanyaji wa data ya COVID-19 unaweza kufungua hali mpya hatari katika ufuatiliaji na ulengaji wa HRD. Kwa mfano, mashirika kadhaa ya haki za kibinadamu yameelezea wasiwasi kuhusu utumiaji vibaya wa programu za kufuatilia waasiliani kwa ufuatiliaji wa waandamanaji, wanaharakati na maandamano na kupelekea ukiukaji wa haki kama vile haki ya ujumuikaji, haki ya kuja pamoja na uhuru wa kusema na kujieleza.


## Tabia na mazoea ya HRD mtandaoni

Mitazamo ya habari za kibinafsi na za kikazi





*Mchoro wa 12: Mtazamo kuhusu habari za kibinafsi na za kikazi*

HRD wana wasiwasi kuhusu ufuatiliaji na faragha mtandaoni, na walichukua tahadhari kubwa kulinda habari yao ya kibinafsi na kikazi. Hata hivyo, wakati wengi walifahamu hatari za kushirikisha ujumbe huu mtandaoni, hii haikuashiria mazoea ambapo HRD bado huchapisha habari zao za kibinafi kwenye mitandao ya kijamii na tovuti za kuungana. Maoni kama hayo yalitolewa mnamo 2018 kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro wa 12B hapa chini. Hii inaonyesha pengo katika habari ambapo licha ya kufahamu changamoto, wengi wa HRD wanakosa maarifa ya kiufundi kuhusu jinsi ya kulinda habari zao.





Mchoro wa 12B: Mitazamo ya habari za kibinafsi na za kikazi (2018)

## Nyayo za dijiti za HRD



Asilimia 57 walisema hawashirikishi maeneo yao ya makazi mtandaoni na asilimia 54 hawashirikishi picha za nyumbani mwao kwenye mitandao ya kijamii. HRD wachache sana walisema wao hushirikisha nambari za simu au kuwezesha wengine kuwatambulisha kwenye mitandao ya kijamii bila idhini yao. Kama mazoea haya yatafanywa kwa mfululizo yanaweza kupunguza hatari na matishio kwa HRD.


## Mazoea na hatua za kiusalama mtandaoni




*Mchoro wa 14: Tabia za kujilinda katika utumiaji wa teknolojia*


Utumiaji wa nywila kulinda rununu ndiyo mazoea maarufu sana ya kiusalama ambayo HRD hufanya ili kujilinda dhidi ya uingiliaji. Hata hivyo, wahojiwa wengi wanaofikia asilimia 43 hawabadilishi nywila kila mara, jambo ambalo huenda likahatarisha usalama wao. Asilimia 48 zaidi hawatumii VPN au usimbaji, ambazo zinapendekezwa sana kwa HRD ili kupunguza tishio la kufunuliwa.

Hali kadhalika, asilimia 53 ya HRD katika uchunguzi wa 2018 walijibu kwamba wao hulinda simu zao za kibinafsi kwa nywila. Kwa ujumla, HRD wanaendeleza tabia nyingine za kugeuza mipangilio ya faragha ili kupunguza ufikiaji na uchakataji wa habari zao, wanakagua habari za kukusanywa na programu na wanatumia zana tofauti kwa mawasiliano ya kikazi na ya kibinafsi.




*Mchoro wa 15: Tabia za kujilinda katika utumiaji wa teknolojia (2018)*

Hata hivyo, HRD wanaonekana kuwa waangalifu kuhusu nyayo za dijiti wanazoacha nyuma.




*Mchoro wa 16: Hatua za Ulinzi Mtandaoni*

# HITIMISHO

Watetezi wa Haki za Kibinadamu katika Kenya wanakabiliwa na hatari zinazoongezeka za ukiukaji wa faragha kama matokeo ya upanuzi wa uwezo wa mawakala wa usalama wa ufuatiliaji, msingi dhaifu wa sheria zinazolinda haki za faragha, utekelezaji duni wa wa masharti na ulinzi wa kisheria na ukusanyaji unaoongezeka wa data ya kibinafsi na serikali na wahusika wasio wa kiserikali. HRD hasa wako katika hali ya hatari kwani baadhi ya kazi zao huenda ikahusisha kupinga mwenendo wa wahusika wenye nguvu ambao wana kichocheo kikubwa cha kulinda masilahi yao. Hii ni pamoja na kupitia utumiaji wa zana za ufuatiliaji ili kutishia na kulenga HRD na wapendwa wao.

Ripoti hii imewasilisha matokeo kuhusu HRD wanaofanya kazi katika sehemu mbalimbali za Kenya juu ya kiwango wanachotambua cha kufunuliwa, uelewa na utambuzi wa ufuatiliaji wa mawasiliano na ufuatiliaji mtandaoni. Ripoti hii pia imetoa uelewa mkubwa wa mikakati ambayo HRD wanatumia kujilinda na kupunguza hatari za ufuatiliaji wa mawasiliano. Hii iliongozwa na maswali ya upana ya uchunguzi kuhusu: ukawaida na misingi ya kisheria inayosimamia haki ya faragha katika Kenya; mitindo inayojitokeza ya serikali na wahusika wasio wa kiserikali kutumia vibaya misingi dhaifu na/au isiyokuwapo ya udhibiti kuendesha ufuatiliaji haramu, sera na mazoea yanayoathiri HRD na kazi yao; vilevile kiwango cha ufunuaji HRD wanachotambua, uelewa na utambuzi wa ufuatiliaji wa mawasiliano; na mikakati ya ulinzi inayotumiwa na HRD.

Wakati HRD walifikia kiwango cha juu kwa ujumla cha ufahamu wa masuala ya ufuatiliaji wa mawasiliano pamoja na kuonyesha wasiwasi kuhusu mawasiliano yanayofanywa kwa sababu za kibinafsi na katika uwezo wao wa kitaalamu ikizingatiwa hali ya shughuli zao, uchunguzi na mahojiano pia yanafichua mapengo kati ya maarifa na mazoea. Kwa hivyo, hata kama baadhi ya HRD waliripoti kuwa na maarifa mengi ya masuala ya mawasiliano, hii si lazima kumaanisha utumiaji wa mazoea bora.

HRD wanafahamu kuhusu vyanzo mbalimbali vya ufuatiliaji, wakitaja matapeli na waingiliaji, huduma za kijasusi na watoa huduma za mawasiliano na intaneti kuwa vyanzo vikuu. Wakati HRD wanachukua hatua fulani kupunguza hatari, inaendelea kuwa ngumu zaidi kupinga wahusika wenye nguvu wa kiserikali na kibinafsi kwa sababu ya ukosefu wa usawa wa mamlaka na rasilimali adimu za HRD za kupinga mazoea yanayotumiwa kuwaweka chini ya ufuatiliaji. Hata hivyo, bado kuna mahitaji ya dharura na muhimu vilevile fursa za kusaidia jamii ya HRD kuelewa vyema na kutumia hatua kadhaa za kupunguza hatari na matishio yanayowakabili.

HRD wameanza kutumia hatua kadhaa za kulinda mawasiliano na habari zao. Hizi

ni pamoja na kupunguza habari za kibinafsi na kikazi zinazotolewa mtandaoni na kwenye mitandao ya kijamii, kulinda vifaa vyao vya kibinafsi kwa nywila, kusimba mawasiliano yao mtandaoni na kugeuza mipangilio ya faragha ili kupunguza ufikiaji na ushirikishaji wa habari zao pamoja na nyingine.

Ikizingatiwa hali ya mageuzi endelevu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kuna haja ya kuwafunza na kuwapatia HRD habari za karibuni zaidi kila wakati kuhusu ulinzi wa habari na mawasiliano yao kulingana na hatari zinazojitokeza. Mbinu hii inapaswa kutofautishwa ikizingatiwa maudhui mahususi na uhalisi ulioshuhudiwa na HRD mbalimbali. Wakati huo huo, kuna haja ya kuendelea kupinga sera na mazoea ya serikali, vilevile yale ya sekta ya kibinafsi.

# Nyongeza ya 1: Orodha Ya Marejesho


Ushirika wa Wanablogu wa Kenya (BAKE) dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 3; Kifungu cha 19 Afrika Mashariki na mwingine(Watu walio na shauku) [2020] eKLR, Ombi Nambari 206 la 2019

Ushirika wa Wanablogu wa Kenya (BAKE), Taarifa kwa vyombo vya habari 7 Mei 2020, https://www.blog.bake.co.ke/2020/05/07/we-have-appealed-the-high-court-decision-on-our-cybercrimes-case/ (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Bygrave, L. A. (2000) Sheria ya ulinzi wa data. Wolters Kluwer Sheria na Biashara, 2002.

Kituo cha Mali ya Kitaalima na Teknolojia ya Habari (2017) "Safaricom na Ugeuzaji wa Trafiki ya Intaneti," Machi 2017, https://blog.cipit.org/wp-content/uploads/2017/03/Final-March-Brief-pages.pdf (Ilifikiwa mnamo 26 Septemba 2020)

Maabara ya Mwananchi (2013) 'Planet Blue Coat: Kuweka Ramani ya Udhibiti wa Kimataifa na zana za Ufuatiliaji, Muhtasari wa Utafiti, Nambari 13, Januari 2013, Chuo Kikuu cha Toronto, Shule ya MUNK ya Masuala ya Kimataifa, https://citizenlab.org/wp-content/uploads/2013/01/Planet-Blue-Coat.pdf (Ilifikiwa mnamo October 2 2020)

Muungano wa Mabadiliko na Demokrasia (CORD) na wengine 2 dhidi ya Jamhuri ya Kenya na wengine 10 [2015] eKLR.

Tume ya Mawasiliano ya Kenya (2012) 'Kenya na ITU zatia saini makubaliano ya kiutawala kwa ajili ya KE- CIRT/CC', 17 Februari, http://www.cck.go.ke/news/2012/KE- CIRT_signing.html (Ilifikiwa mnamo 17 Januari 2018)

Daily Nation. (2014,). "Kwa nini Ikulu ilimpigia simu mkuu wa Safaricom kuhusu ukosefu wa usalama," Daily Nation, Mei 13, www.nation.co.ke/news/Why-State-House-made-a-call-to-Safaricom-chief-over-insecurity/-/1056/2313756/-/ybd3dt/-/index.html (Ilifikiwa mnamo 7 Novemba 2018)

Kituo cha Ulaya cha Uzuiaji na Udhibiti wa Magonjwa (2020) Ufuatiliaji wa waasiliani kwa ajili ya COVID-19: ushahidi wa sasa, machaguo ya kuimarisha na kutathmini rasilimali zinazohitajika, Ripoti ya Kiufundi, Aprili 2020, ukurasa wa 5

Huawei, "Ufuatiliaji wa Video kama Msingi wa "Mji Salama" katika," https://www.huawei.com/ke/industry-insights/technology/digital-transformation/video/video-surveillance-as-the-foundation-of-safe-city-in-kenya (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Shirika la Kutetea Haki za Kibinadamu (2017) "Haistahili Hatari" Matishio ya Uhuru wa Kujieleza Kabla ya Uchaguzi wa Kenya wa 2017," https://www.hrw.org/sites/default/files/report_pdf/kenya0517_web.pdf (Ilifikiwa mnamo Septemba 2020)

Kapiyo, V. na Githaiga, G. (2014) 'Je, ufuatiliaji ni suluhisho la matishio ya kiusalama

Kenya?', https://giswatch.org/en/country-report/communications-surveillance/kenya (Ilifikiwa 2 Oktoba 2020)

Kenya COVID-19 Tracker, https://play.google.com/store/apps/details?id=org.medicmobile.webapp.mobile.surveillance_covid19_kenya&hl=en&gl=US (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Mtandao wa Kisheria na Kimaadili juu ya HIV na UKIMWI (KELIN) na wengine 3 dhidi ya Katibu wa Baraza Wizara ya Afya na wengine 4 [2016] eKLR

Maono ya 2030 ya Kenya, http://www.vision2030.go.ke/about-vision-2030/ (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Marczak, B., Scott-Railton, J., McKune, S., Abdul Razzak, B. na Deibert, R. (2018) Kibemasa: Ufuatiliaji wa Shughuli za Programu ya Kiujasusi ya NSO Group ya Pegasus katika nchi 45, Ripoti nambari 113 ya Utafiti wa Maabara ya Mwananchi, Chuo Kikuu cha Toronto, Septemba 2018.

Medic Mobile (2020). "Habari Mpya Kuhusu COVID-19: programu inayoendeshwa na CHT inasaidia ufuatiliaji wa COVID-19 katika Kenya," 30 Aprili, April, https://medicmobile.org/blog/covid-19-update-community-health-toolkit-cht-powered-app-supporting-covid-19-surveillance-in-kenya (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

mHealth Kenya (2020) "Ufuatiliaji wa Afya ya Umma na Mifumo ya Uitikiaji," https://www.mhealthkenya.org/covid-19 (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Muungano wa Kitaifa wa Watetezi wa Haki za Kibinadamu-Kenya (NCHRD-K), Mtandao wa Masuala ya Kisheria na Kimaadili Kenya na Mtandao wa Masuala ya Kimaadili juu ya HIV na Ukimwi (KELIN), Mpango wa Paradigm, na Privacy International (2019) Haki ya Faragha katika Kenya, Upitiaji wa Kimataifa wa Ripoti ya Pamoja Kipindi cha 35 –Kenya, Juli 2019, ukurasa wa 8

Huduma ya Kitaifa ya Polisi (2019) usalama waimarishwa Mombasa, 5 Septemba. http://www.nationalpolice.go.ke/2015-09-08-17-56-33/news/297-surveillance-heightened-in-mombasa.html (Ilifikiwa mnamo 2 Oktoba 2020)

Needham, Roger M., na Michael D. Schroeder. "Kutumia usimbaji kwa uthibitishaji katika mitandao mikubwa ya kompyuta." Mawasiliano ya ACM 21.12 (1978): 993-999.

Nowak, M. (1993) U.N. Agano Kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa: Ufafanuzi wa CCPR, (toleo la 2) Kehl am Rhein, Ujerumani; Arlington, VA: N.P. Engel Publishers.

Jukwaa la Haki za Wanubi na wengine 2 dhidi ya Mkuu wa Sheria na wengine 6; Jamii ya Masilahi ya Watoto na wengine 9 (Watu walio na Shauku) [2020] Omnbi la Petition 56, 58 na 59 la 2019 (Limejumuishwa) eKLR

Parkinson, J., Bariyo, N. na Chin, J. (2019) "Mafundi wa Huawei Walisaidia Serikali za Kiafrika Kupeleleza Wapinzani wa Kisiasa," Wall Street Journal, 15 Agosti, https://www.wsj.com/articles/huawei-technicians-helped-african-governments-spy-on-political-opponents-11565793017 (Ilifikiwa mnamo 21 Septemba 2020)

Brigedi za Amani za Kimataifa (2012) Tathmini ya uwezekano na ufanisi wa msindikizo wa kiulinzi katika Kenya https://peacebrigades.org.uk/fileadmin/user_files/international/files/special_report/PBI_Kenya_report.pdf (Ilifikiwa mnamo 21 Septemba 2020)

Privacy International (2017) Fuatilia, Kamata, Ua: Ndani ya Ufuatiliaji wa Mawasiliano na Kukabiliana na Ughaidi katika Kenya

Privacy International, 'Ufuatiliaji wa Mawasiliano. Video: Ufuatiliaji Wa Mawasiliano Ni Nini?' https://privacyinternational.org/explainer/1309/communications-surveillance (Ilifikiwa mnamo 21 Septemba 2020)

Privacy International, (2006) Faragha na Haki za Kibinadamu 2006: Uchunguzi wa Kimataifa wa Sheria na Maendeleo ya Faragha.

Ushuhuda wa Steve Feldstein (2020) mbele ya Usikilizwaji wa Tume ya Upitiaji wa Uchumi na Usalama wa Marekani-China kuhusu Malengo ya Kimkakati ya China katika Afrika

Mei 8, 2020, ukurasa wa 4.

Kamati ya UN ya Haki za Kibinadamu (1998) Maoni ya Jumla ya CCPR Nambari 16: Kifungu cha 17 (Haki ya Faragha), Haki ya Kuheshimiwa kwa Haki ya Faragha, Familia, Nyumbani na Mawasiliano, na Ulinzi wa Heshima na Sifa, 8 Aprili 1988, https://www.refworld.org/docid/453883f922.html (ilifikiwa mnamo 19 Oktoba 2020)

Umoja wa Mataifa (2013) 'Ripoti ya Mwanahabari Maalum juu ya ukuzaji na ulinzi wa haki ya uhuru wa maoni na kujieleza, Frank La Rue' A/HRC/23/40, 17 Aprili 2013' A/HRC/23/40, 17 April 2013, http://www.humanrights.is/en/human-rights-education-project/comparative-analysis-of-selected-case-law-achpr-iachr-echr-hrc/the-right-to-respect-for-private-and-family-life/what-is-private-life (Ilifikiwa mnamo 18 Oktoba 2020)

Kamati Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa (2004) Maoni ya Jumla Nambari 31 [80] Hali ya Wajibu wa Kijumla wa Kisheria Uliowekwa kwa Nchi Zilizo Washiriki wa Aganot, 29 Machi 2004 (mkutano wa 2187), CCPR/C/21/Rev.1/Add. 13, aya ya 6

Tume ya Sheria ya Kivictoria katika Australia (2001) 'Sheria ya Faragha: Machaguo ya Mabadiliko', Gazeti la Habari, www.lawreform.vic.gov.au (Ilifikiwa mnamo 16 Novemba 2018)

# NYONGEZA YA 2: Dodoso la Uchunguzi

## UCHUNGUZI WA UFUATILIAJI WA MAWASILIANO WA WATETEZI WA HAKI ZA KIBINADAMU (HRD)

| | |
|---|---|
| Jina la Mhoji: | |
| Msimbo wa Mhoji: | |
| Wakati wa Kuanza: | Wakati wa Kumaliza: |
| Tarehe ya Mahojiano: | |

**Utangulizi na hati ya idhini**

- Msalimie mtu unayemhoji, na ujitambulishe kama unayeendesha uchunguzi kwa niaba ya Muungano wa Watetezi.
- Elezea lengo la utafiti: Uchunguzi huu ni wa utafiti ambao unakagua athari za ufuatiliaji wa mawasiliano na faragha kwa watetezi wa haki za kibinadamu katika Kenya.
- Uliza kama mtu unayezungumza naye ana maswali yoyote kwako kabla ya kuendelea.
- Uliza kama ni wakati unaofaa – kama sivyo, unaweza kupiga simu tena wakati unaofaa.
- Uliza kama mhojiwa yuko radhi kuhojiwa.
- Mjulishe kwamba majibu ya uchunguzi huu yatawekwa kwa usiri. “Hakuna atakayejulishwa kwamba ulishiriki katika uchunguzi huu au una ufikiaji wa habari ulizotoa, isipokuwa Muungano wa Watetezi. Jina lako halitatumika au kuonekana katika sehemu yoyote ya uchunguzi huu. Una haki ya kusimamisha mahojiano wakati wowote au kuruka swali lolote ambalo hutaki kujibu.”
- Akikubali, anzisha mahojiano. Ikiwa mhojiwa hayuko tayari, usiulize swali jingine na usonge mbele kwa mtu anayefuata.

SEHEMU YA I: HABARI ZA KIBINAFSI

| | | |
|---|---|---|
| | Kitambulisho cha Mhojiwa (k.m. 001, 0024 n.k.) | |
| 1. | Umri | ❑ 18-30<br>❑ 31-40<br>❑ 41-50<br>❑ 50 and above |
| 2. | Jinsia (soma kwa sauti) | Natambua jinsia yangu kamaÉ<br>❑ Mwanaume<br>❑ Mwanamke<br>❑ Jinsia isiyo thabiti/Si Kike au Kiume<br>❑ ______ (jaza pengo)<br>❑ Napendelea kutoÞchua |
| 3. | Kiwango cha Juu Zaidi cha Elimu | ❑ Sekondari/Shule ya Upili<br>❑ Chuo/Chuo Kikuu Cheti/Diploma<br>❑ Digrii ya Kwanza<br>❑ Digrii ya Uzamili<br>❑ Digrii ya Uzamivu |
| 4. | Miaka ya Tajiriba katika kazi ya HRD | ❑ Chini ya Mwaka Mmoja<br>❑ 1-5<br>❑ 6-10<br>❑ 11 na juu |
| 5. | Una uhusiano na shirika? | ❑ Ndiyo<br>❑ La |
| 6. | Ni masuala gani [yanayohusiana na haki za kibinadamu] umekuwa ukishughulikia? (majibu anuwai) | ❑ Serikali/Uongozi<br>❑ Jinsia/Haki za Wanawake<br>❑ Kupinga Ulanguzi/Uhamiaji<br>❑ Uhamisho<br>❑ Mazingira<br>❑ Uhuru wa Kujieleza<br>❑ Uhuru wa kujumuika<br>❑ Haki za Watoto<br>❑ Haki za Leba<br>❑ Wakimbizi<br>❑ Mengineyo (ashiria) |

| Dhana Muhimu | |
|---|---|
| 7. | Unaposikia maneno UFUATILIAJI WA MAWASILIANO, ni MANENO gani huja akilini mwako (Andika mawili, neno moja moja pekee)<br>• ________________<br>• ________________ |
| 8. | Unaposikia maneno FARAGHA YA MAWASILIANO, ni MANENO gani huja akilini mwako (Andika mawili, neno moja moja pekee)<br>• ________________<br>• ________________ |
| 9. | Unaposikia maneno USALAMA WA MAWASILIANO, ni MANENO gani huja akilini mwako (Andika mawili, neno moja moja pekee)<br>• ________________<br>• ________________ |

| | Ufahamu wa taratibu na majukwaa ya ukusanyaji wa data | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10. | Kwa ujumla, unakadiriaje kiwango chako cha ufahamu/maarifa ya matishio na hatari zinazotolewa na yafuatayo katika ufuatiliaji (Kwa kipimo cha 0-5 ambapo 0 ni Hakuna Maarifa na 5 ni Juu Sana) | Hakuna Maarifa | Chini Sana | Chini | Wastani | Juu | Juu Sana |
| | | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mifumo ya Nafasi ya Kimataifa (GPS) | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ukusanyaji wa biometriki | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Televisheni ya Mzunguko Iliyofungwa (CCTV) | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ufuatiliaji mtandaoni | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ufuatiliaji wa waasiliani kutumia rununu | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| | Ufahamu wa ufuatiliaji wa mawasiliano | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Kadiria maarifa yako kuhusiana na vipengele vifuatavyo (Kwa kipimo cha 0-5 ambapo 0 ni Hakuna Maarifa na 5 ni Juu Sana) | Hakuna Maarifa | Chini Sana | Chini | Wastani | Juu | Juu Sana |
| | Maarifa yako kwa jumla kuhusu ufuatiliaji wa mawasiliano | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Zana zinazotumiwa na serikali kwa ufuatiliaji wa mawasiliano | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ufahamu kuhusu ufuatiliwaji wa habari/data na serikali | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ufahamu kuhusu ukusanyaji wa habari za kibinafsi na serikali | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Ufahamu kuhusu ukusanyaji wa habari za kibinafsi na kampuni za kibinafsi | 0 | | | | | |
| | Jinsi ya kuhifadhi habari/data ya kibinafsi kwa usalama | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Njia ambazo kwazo utumiaji wangu wa intaneti unaweza kufuatiliwa na serikali | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Njia ambazo kwazo simu yangu inaweza kuingiliwa | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| 12. | Kadiria maswali yafuatayo kuhusu Ufuatiliaji wa Mawasiliano (Kwa kipimo cha 1-5 ambapo 1 ni Nakataa Kabisa na 5 ni Nakubali Kabisa) | Nakataa Kabisa | Nakataa | Upande Wowote | Nakubali | Nakubali Kabisa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nina wasiwasi kuhusu ufuatiliaji mtandaoni | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Nina wasiwasi kuhusu faragha ya habari zangu za kibinafsi na kikazi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Natambua athari hasi za ushirikishaji wa habari mtandaoni | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Nina imani kwamba ni mimi tu niliye na ufikiaji wa habari kwenye vifaa vyangu vyote k.m. kompyuta, rununu, baruapepe, kipakatalishi, kibao n.k. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wakati mwingine mimi hushirikisha habari zisizo sahihi kunihusu mtandaoni ili kujilinda | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mimi hushirikisha habari za kibinafsi kwenye tovuti za intaneti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mimi hushirikisha habari za kibinafsi kwenye tovuti za kijamii k.m. Facebook, Twitter, Instagram | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| Vyanzo VYA UFUATILIAJI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 13. | Unadhania kwa kadiri gani kwamba wafuatao wanataka kufikia taarifa zako za kibinafsi?(Kwa kipimo cha 1-5 ambapo 1 ni Haiwezekani Kamwe na 5 ni Uwezekano Mkubwa) | Hakuna Uwezekano Kamwe | Hakuna Uwezekano | Labda | Kuna Uwezekano | Kuna Uwezekano Mkubwa |
| | Polisi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mawakala wa ujasusi k.m. NIS | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kampuni/Mashirika ya kibinafsi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Watoa huduma za mawasiliano/intaneti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mwajiri | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wahalifu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Jamaa | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Marafiki | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wahusika wengine (matapeli, waingiliaji) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | | | | | | |
| 13b | Unafikiri kwa kadiri gani kwamba wafuatao wanafuatilia habari zako za kibinafsi? (Kwa kipimo cha 1-5 ambapo 1 ni Haiwezekani Kamwe na 5 ni Uwezekano Mkubwa) | Hakuna Uwezekano Kamwe | Hakuna Uwezekano | Labda | Kuna Uwezekano | Kuna Uwezekano Mkubwa |
| | Polisi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mawakala wa ujasusi k.m. NIS | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kampuni/Mashirika ya kibinafsi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Watoa huduma za mawasiliano/intaneti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Mwajiri | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wahalifu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Jamaa | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Marafiki | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wahusika wengine (Matapeli, waingiliaji) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| UTAMBUZI WA USALAMA WA ZANA ZA MAWASILIANO | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Kwa maoni yako, njia zifuatazo za mawasiliano ni salama kwa kadiri gani? (Kwa kipimo cha 1-5, ambapo 1 ni Si Salama Kamwe na 5 ni Salama Sana) | Si Salama Kamwe | Si Salama | Salama Kiasi | Salama | Salama Sana |
| | Kuzungumza ana kwa ana | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kutumia simu ya waya | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kupiga simu kutumia simu yako | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kutuma arafa | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kutuma baruapepe bila usimbaji | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kutumia soga za rununu zilizosimbwa (WhatsApp, Signal) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kutumia soga na jumbe za papo hapo (k.m. Google, Yahoo) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kuchapisha kwenye mitandao ya kijamii (Facebook, Twitter, Instagram) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15. | Una sababu yoyote ya kuamini kwamba huenda lolote kati ya yafuatayo lilikutendekea? | Ndiyo | La | Alikataa Kujibu |
| | Baruapepe yako ishaingiliwa awali | 1 | 2 | |
| | Simu yako ishaunganishwa kisiri awali | 1 | 2 | |
| | Akaunti yako ya mitandao ya kijamii ishaingiliwa awali | 1 | 2 | |

| TABIA ZA USALAMA MTANDAONI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Unatumia mazoea yafuatayo kwa kadiri gani? | Hakuna | Wakati Mwingine | Nadra | Mara Nyingi | Kila Wakati |
| | kutumia zana tofauti za mawasiliano kwa watu/kazi tofauti kwa sababu za kiusalama | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kugeuza mipangilio yako ya usalama ili kupunguza wale ambao wanaweza kufikia/kutumia habari zako za kibinafsi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kukagua ni aina gani ya habari zitakusanywa kabla ya kusakinisha program kwenye kifaa chako maizi (simu au kibao) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kukubali/kukataa simu na kompyuta kama mchango kutoka kwa wahusika wa tatu | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kulinda au kuficha mawasiliano ya mtandaoni k.m. kwa usimbaji wa baruapepe/diski ngumu, utumiaji wa VPN | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kutumia nywila kufunga simu yako kila wakati | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | kubadilisha nywila yako kila wakati | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 17. | Tafadhali niambie jinsi unavyokubaliana au kutokubaliana na kauli zifuatazo kuhusu tabia za Mtandaoni?<br><br>(Kwa kipimo cha 1-5 ambapo 1 ni Nakataa Kabisa na 5 ni Nakubali Kabisa) | Nakataa Kabisa | Nakataa | Upande Wowote | Nakubali | Nakubali Kabisa |
| | Wewe hulinda maudhui ya baruapepe yako na tabia za uvinjari dhidi ya watangazaji na wahusika wa tatu yaani kwa kudhibiti vidakuzi vya wavuti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Kwa ujumla, una wasiwasi kuhusu viwango vyako vya sasa vya ulinzi wa faragha na ISP, baruapepe na wavuti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Wewe husoma na kuelewa mikataba ya mtumiaji na masharti ya huduma kabla ya usajili kwenye tovuti zozote za intaneti na mitandao ya kijamii | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Umebadilisha tabia zako mtandaoni kwa sababu ulifikiri mawasiliano yako yalikuwa yakifuatiliwa | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| Sheria ya Ulinzi wa Data | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20 | Unafahamu kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2019?<br>Ndiyo<br>La<br>Kama ni La, komesha mahojiano. Kama ni Ndiyo, nenda kwenye swali linalofuata… | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21. | Sheria ya Ulinzi wa Data, 2019 hudhibiti ukusanyaji na uchakataji wa data katika Kenya. Huanzisha ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data, ambayo itaongozwa na Kamishna wa Data. Je, unafahamu majukumu ya ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Data? | Nafahamu | Sifahamu | Alikataa Kujibu |
| | | 1 | 2 | 3 |
| | | 1 | 2 | 3 |
| | | 1 | 2 | 3 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22. | Kama ndiyo, ni majukumu gani unayoyafahamu? (Usisome kwa sauti; weka alama kwa yote) | Ndiyo | La | Alikataa Kujibu |
| | Kusimamia utekelezaji wa Sheria | | | |
| | Kuanzisha na kudumisha rejesta ya wadhibiti wa data na wachakataji wa data | | | |
| | Kusimamia shughuli za uchakataji wa data | | | |
| | Kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote na mtu yeyote kuhusu ukiukaji wa haki zake chini ya Sheria hiyo | | | |
| | Jingine (Aini) | | | |

## Biometriki

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 23 | Ulijisajili kwa Huduma number? | Ndiyo | La | Alikataa kujibu |
| | | | | |
| 23b | Kama la, ni kwa nini hukujisajili kwa Huduma Number? (Usisome kwa sauti, majibu mseto yanawezekana) | Ndiyo | La | Alikataa kujibu |
| | Nilihisi kwamba ilitoa tishio kwa faragha yangu | | | |
| | Nilihisi habari za kibinafsi zilizohitajika zingeweza kupelekea ufuatiliaji na utazamaji wa kazi yangu ya HRD | | | |
| | Sikukubaliana na viendeshi na nia zake za kisiasa | | | |
| | Sikuwa na habari kuhusu zoezi la usajili wa Huduma Number | | | |
| | Sikuweza kujisajili ndani ya siku usajili ulipoendelea | | | |
| | Hakukuwa na vituo vya usajili katika eneo langu | | | |
| | Nyingine (Aini) | | | |

## Ufuatiiliaji wa Covid-19

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 24. | Umepokea jumbe/arifa/taarifa kuhusiana na janga la covid-19, ambazo hujajisajili kwazo? | Ndiyo | La | Alikataa kujibu |
| | | 1 | 2 | 3 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 25. | Unafahamu kuhusu majaribio yoyote ya serikali ya Kenya kufanya ufuatiliaji wa simu kwa watu ambao wamepimwa COVID-19? | Nafahamu | Sifahamu | Alikataa kujibu | Sijui |
| | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 26. | Kama ndivyo, unaamini kwa kadiri gani kwamba ufuatiliaji wa COVID-19 na serikali kutumia rununu unaingilia faragha?<br>(Kwa kipimo cha 1-5 ambapo 1 ni Chini Sana na 5 ni Juu Sana) | Chini Sana | Chini | Wastani | Juu | Juu Sana |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 27. | Unatumia programu zozote za rununu ambazo hukusanya data au kukuwezesha kuripoti kuhusu hali yako ya COVID-19? | Ndiyo | La | Alikataa kujibu |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 28. | Kama ndivyo hapo juu (swali la 27), aini jina la programu. (usisome kwa sauti) | Ndiyo | La | Alikataa kujibu |
| | Jitenge | 1 | 2 | 3 |
| | Medic Mobile | | | |
| | Nyinginezo | | | |

| 29. | Una imani kiasi gani kwamba data yako ya kibinafsi iliyokusanywa kama sehemu ya hatua za kushughulikia janga la COVID-19...<br><br>(Kwa kipimo cha 0-5 ambapo 0 ni Hakuna na 5 ni Juu Sana) | Hakuna | Chini Sana | Chini | Wastani | Juu | Juu sana |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Itahifadhiwa salama na serikali ya Kenya? | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| | Itatumiwa na serikali pekee kwa madhumuni ya uzuiaji na udhibiti wa COVID-19? | 0 | | | | | |
| | Itahifadhiwa salama na mashirika k.m kliniki/hospitali za kibinafsi? | 0 | | | | | |
| | Itatumiwa na mashirika pekee kwa madhumuni ya uzuiaji na udhibiti wa COVID-19? | 0 | | | | | |

| 30. | Ni nani unayemwamini kuwa na ufikiaji wa data yako iliyokusanywa kutoka kwa programu ya ufuatiliaji wa waasiliani ya COVID-19? | Ndiyo | La | Alikataa kujibu | Sijui |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | | | | |
| | Kampuni za kibinafsi | | | | |
| | | | | | |
| | Hakuna hata moja | | | | |
| | Nyingine | | | | |

# NYONGEZA YA 3: Mwongozo wa Mahojiano ya Kisifa

Twambie kwa kifupi kukuhusu na kazi yako kama Mtetezi wa Haki za Kibinadamu.

Kama HRD, una wasiwasi gani kuhusu ufuatiliaji wa mawasiliano?

Ni nini unachoona kama vyanzo vya ufuatiliaji katika kazi yako kama HRD?

Ni hatua gani za ulinzi ambazo umeanza kutumia ili kuhakikisha usalama na faragha ya mawasiliano yako? Na kwa nini?

Ushawahi kuwa chini ya aina yoyote ya ufuatiliaji wa mawasiliano kwa sababu ya kazi yako? Kama ndivyo, elezea kilichotokea...

Ni masuala gani ya ufuatiliaji/faragha ya mtandaoni unayoyafahamu? Unawezaje/ unapaswa kuyashughulikia namna gani?

Kuna athari gani za ufuatiliaji na faragha ya mawasiliano kwa watetezi wa haki za kibinadamu katika Kenya?

Katika kiwango cha shirika – Ni hatua gani umechukua ili kulinda mawasiliano na habari zako?

Unaamini kwa kadiri gani kwamba ufuatiliaji wa COVID-19 na serikali kutumia rununu unaingilia faragha yako? Na kwa nini?

Una wasiwasi gani kuhusu Huduma Number na faragha ya kazi yako kama HRD?

DEFENDERS
COALITION

**SAFETY, SECURITY, WELLBEING OF HRDS**

Defenders Coalition | P. O. Box 26309- 00100 Nairobi
info@defenderscoalition.org | +254 712 632 390 | www.defenderscoalition.org